SportPesa
TZS. 576,086,780
BET LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



**TCU** yafungua dirisha la mwisho udahili wanafunzi wa shahada ya kwanza

UKURASA 3


Nipashe

TESA

Jumanne Oktoba 12, 2021

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Mzee Mwakangale; alianza shule ukoloni, digrii miaka 10 ya Nyerere

Ukurasa 14

Kinababa walivyo muhimu kuwaepushia mabinti mimba

Ukurasa 12

ELIMU
NA PETER ORWA

MIAKA 22 BILA NYERERE;

Namna alivyokokotoa elimu tangu zama Tanganyika hadi kung'atuka

• UPE kung'ara' Afrika; wasomi, JKT; robo ya bajeti elimu

UKIMCHAMBUA mara tu baada ya kupata nafasi ya uongozi wa nchi, Waziri Mkuu wa Tanganyika na baada ya mwaka mmoja Rais, Baba wa Taifa Julius Nyerere, hajawahi kuwa mbali na fani yake ya ualimu.

Baada tu ya kukalia kiti, mpango wake wa kwanza wa muda mfupi wa maendeleo wa miaka mitatu hadi 1964, kati ya aliyoyapa kipaumbele ni elimu. Mara baada ya Uhuru wa Tanganyika, alifuta elimu ya matabaka, ambapo jamii ya kizungu walipewa nafasi kubwa, kufuatiwa na Waasia kisha Waafrika, ikawa sawa kwa wote.

Mzizi wa shule za sekondari kihistoria, nyingi zilizotoka mikononi mwa ukoloni, zikibeba ishara za matabaka, mathalan jijini Dar es Salaam kuna shule kama St. Xavier ambayo leo ni Kibasila; St Francis, leo ni Pugu na hata iliyokuwa Forodhani .

Pia, shule kama hizo za kihisitoria za wasichana jijini, zimo Jangwani, Zanaki na Kisutu, huku za wavulana ni Tambaza na Azania.

Nje ya jiji kuna shule kama Minaki (Kisarawe), Ihungo na Nyakato (Kagera), Mazengo (Dodoma), Mzumbe (Morogoro), Galanos (Tanga), Alliance (Musoma Sekondari) na Malangali (Iringa).

**UWEKEZAJI RASMI**

Mwaka 1964, Tanzania ikiwa rasmi katika mfumo wa Muungano, Nyerere aliwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye elimu na kudumu daima kama dira ya maendeleo ya kitaifa hadi sasa.

Mpango huo wa kwanza wa miaka mitano 1964 - 1969, dhima ilikuwa ni kuwatoa Watanzania katika mfumo tegemezi. Mwalimu Nyerere, aliamini elimu ingewafikisha katika ukombozi kamili.

Kwa kipindi cha miaka mitatu ya baada ya uhuru, watoto wa Kitanzania hawakupata elimu ya msingi, ama kwa kukosa nafasi kutokana na nafasi chache au kutokana na upeo duni wa haja ya kutumia nafasi hiyo. Hivyo, mpango ulilenga kupatikana shule kwa wastani kila kijiji, ikizingatiwa asilimia 90 ya Watanzania walioishi vijijini.

Ili kufanikisha hilo, mbinu iliyotumika ni falsafa ya kijamaa, iliyokuwa ni itikadi ya nchi, Tanzania ikiwa na chama kimoja tangu 1964, wananchi walishirikishwa kwenye ujenzi, kama ilivyo katika ujenzi wa sekondari za kata unaoendelea sasa.

Ndani ya mpango huo wa miaka mitano, hadi kutimu mwaka 1967, msukumo mkubwa ulitoka katika Azimio la Arusha, uliofikiwa na chama tawala TANU kikiipa tafsiri 'Namna ya kipekee ya kuufanikisha Ujamaa.'

Mwaka 1966, uongozi wa Mwalimu Nyerere, uliona haja ya vijana nchini kuishiriki mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kisheria kwa wahitimu wa kidato cha nne na kupata mafunzo zaidi ya mwaka mmoja au zaidi, kupata vijana bora wa kutumikia taifa kwa moyo, imani na stadi sahihi.

Sio kwamba ilipitia salama, bali ilipata mabishano kwa baadhi ya vijana kutokukubali, lakini ilitekelezeka kisheria kwa maana ya kuunda mwelekeo wa kujenga kitaifa. Ni wakati ambao Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kilishaanza.

Hadi hatua ya miaka 10 ya Uhuru, ambayo Mwalimu Nyerere alijisifu kuwapo maendeleo makubwa baada ya Tanzania huru, ulikuwa umeshapita mwaka mmoja kuanza Mpango wa Maendeleo wa Pili kitaifa, 1969 hadi 1974.

Tangu kupatikana uhuru wa nchi, eneo mojawapo lilibainika kuwa na pengo ni wataalamu.

Rais Nyerere, alitumia mbinu ya Serikali ya Tanganyika na baadaye Tanzania kujenga urafiki na nchi zingine zilizopiga hatua, zikiwapatia vijana nchini, fursa kwenda kusoma Ughaibuni.

Mfano hai ni wataalamu wa uhasibu kwenda kujifunza uhasibu (kama CPA), Associated Chartered Certified Accountancy (ACCA) na Associated Certified Accountancy (ACA), Uingereza, madaktari na fani nyinginezo nchini Cuba, China na iliyokuwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Urusi (USSR); askari na wanahabari na katika vyuo vikuu vya Sandhurst na Cardiff, Uingereza.

**YA AZIMIO MUSOMA**

Ndani na mpango huo wa pili, 1969 hadi 1974, mengi yalishuhudiwa katika sekta ya elimu, ambayo Mwalimu Nyerere katika uongozi wake wa TANU na serikali aliundia dira na msukumo.

Ilifika kipindi elimu iliwekewa mapinduzi makubwa, ikiwamo kuchukua hisa kubwa zaidi katika bajeti ya nchi, kuna wakati alitengea asilimia 20 hadi 25 ya bajeti yote.

Mwaka 1974, Mwalimu Nyerere kupitia kofia yake ya uwenyekiti wa TANU akawezesha kupitishwa mpango, ambao mantiki yake ya kina, una wajihi wa kuendeleza Azimio la Arusha la mwaka 1967.

Hapo kuliundiwa tamko: Azimio la Musoma, lililohimiza kuboresha elimu kwa wote. Ndani pameshuhudiwa mengi kuhakikisha shule za msingi kila kijiji, wazo lililoanza katika mpango wa kwanza, 1964.

Mwalimu Julius Nyerere, katika moja ya mahafali ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam – Morogoro (sasa SUA). **PICHA: MTANDAO**

**INAENDELEA UK.12**

**Nipashe**
Jumanne Oktoba 12, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580731
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# Samia: Nitatumbua bila kuangalia kabila la mtu

UKURASA 2



Wananchi wa Kijiji cha Kibingo wilayani Kibondo mkoani Kigoma wakisubiri kupata chanjo ya UVIKO-19 baada ya kuhamasika kutokana na kampeni iliyofanyika hivi karibuni. **PICHA: ADELA MADYANE**

## CHADEMA yampa masharti 3 Msajili



UKURASA 2

UKURASA WA 3

### HISTORIA YA NYERERE KUFUNDISHWA SHULE 120

SHULE 120, jijini Dar es Salaam, zimealikwa nyumba ya Makumbusho kuwawezesha wanafunzi kujifunza kivitendo historia ya Baba wa Taifa, Hayati ...

UKURASA WA 3

### RAIS MWINYI AITAKA EAC KUPITIA SERA SEKTA UTALII

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezitaka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kufanya mapitio...

UKURASA WA 8

### WATATU WAFARIKI KWENYE AJALI AKIWAMO MSTAAFU

WATU watatu wamefariki dunia akiwamo mstaafu aliyekuwa akienda kuwaaga watumishi wenzake baada ya kustaafu...
kazi.

## RIPOTI MAALUM

# Madaktari watoa ushuhuda corona

UKURASA 7

**MICHEZO** GOMES AHOFIA MUGALU, SAKHO KUIKOSA GALAXY UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga (watatu kulia), akizungumza baada ya kuzindua maandalizi ya kongamano la uwekezaji kwenye sekta ya misitu. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Saady Mtambule, Mkuu wa Wilaya ya Itinga Mjini, Mohamed Moyo (wapili kushoto), wapili kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Peres Magiri na Mbunge wa Viti Maalum Iringa, Rita Kabati. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia: Nitatumbua bila kuangalia kabila la mtu

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema atamtumbua kiongozi yeyote aliyeteuliwa na kushindwa kutekeleza majukumu yake bila kuangalia ni wa kabila gani.

Rais Samia alibainisha hayo jana baada ya kuwaapisha viongozi aliowateua kushika nafasi mbalimbali katika viwanja vya Ikulu Chamwino, jijini hapa.

"Mimi ninakotoka hakuna makabila na tumshukuru Baba yetu wa Taifa Mwalimu Nyerere, ametukuza bila kuangalia makabila yetu mimi pia nipo hapa bila kuangalia kabila sasa wapo watu hapa ukiwashika wamefanya makosa ukiwawajibisha wanadai nimewajibishwa kwa sababu ya kabila.

"Mimi hapa ukiniuliza kabila langu nani nitakwambia mimi ni Mzanzibar sina kabila na kwa maana hiyo hata katika utendaji wangu wa kazi sina kabila uwe Mmakonde uwe mnini, ukikosea kwenye kazi ni mimi na wewe wala sitakufumbia jicho, sasa kama umetoka ulikotoka ukatumbuliwa unasema mimi ni wa kabila fulani hiyo sumu mnaepeleka sana nawaomba msimame," alionya Rais Samia.

Aidha, alisema yeye hana kabila kwa kuwa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliwafundisha kufanya kazi bila kuangalia makabila ya watu na ndicho anachokifanya na kuwataka wateule waende kufanya kazi.

"Tena jana (juzi) hili nilisahau kulisema angalieni kwa kipindi hicho tulitumbua wangapi na mimi kwa miezi sita nimetumbua wangapi na angalieni waliongia ni makabila mangapi nimetumbua.

"TAMISEMI kwa mfano kuna wa-Tanga wangapi, waziri ni m-Tanga Katibu mkuu ni m-Tanga hadi nikaambiwa kuwa unajua hapa mheshimiwa umekosea umepanga wa-Tanga tupu nikasema waacheni wafanye kazi wakilikoroga nitawatumbua na katika maeneo mengine ni hivyo sipangi watu kwa makabila yao," alisisitiza Rais Samia.

Kadhalika, aliwataka wakuu wa mikoa kufanya kazi zao kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni la kuacha tabia za kuwa waungu watu katika maeneo yao.

"Uongozi ni dhamana sio zawadi, hivyo kuna miiko yake na kanuni, sitegemei wala kuona, wakuu wa mikoa kuwa waungu watu sio watu wawatumikie nyie bali nyie ndiyo mnapaswa kuwatumikia watu, sitegemei kuona mkuu wa mkoa kuwa mfano mbaya wa kuongoza watu sita kuwa mstahimilivu katika tabia hiyo," alisema.

Vilevile, aliagiza Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhakikisha fedha zinazotolewa hivi sasa na serikali zinasimamiwa ili kuleta tija katika miradi iliyokusudiwa.

"Hizi fedha ambazo zinamiminika katika maeneo mbalimbali nchini siziwafanye watu wa halmashauri kubweteka katika ukusanyaji wa mapato kwani changamoto bado zipo nyingi muendelee kukusanya mapato na uwezo huo mnao," alisema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alimshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha nyingi za utekelezaji wa miradi na kuahidi kwenda kuzisimamia ipasavyo.

Alisema katika ujenzi wa vyumba vya madarasa wamepokea na leo watatoa mkeka wa mgawanyo wa fedha hizo za vyumba vya madarasa kwa kila mkoa umepata madarasa mangapi kulingana na idadi ya wanafunzi wanaotegemewa kujiunga na kidato cha kwanza kulinganisha na idadi ya wanafunzi waliomaliza kidato cha nne.

"Ile 'Gap' ndiyo itatupa picha ya madarasa mangapi yanayohitajika ila nikuhakikishie Mheshimiwa Rais hakuna halmashauri itakayokosa mgao wa vyumba vya madarasa," alisema.

Alisema katika sekta ya afya kwa Mkoa wa Shinyanga kuanzia Julai hadi Septemba fedha zilizopelekwa ni Sh. bilioni 5.2 ambazo zinaenda kujenga zahanati 24, vituo vya afya sita na hospitali za wilaya tano.

"Upande wa TARURA bajeti ya Mkoa wa Shinyanga kwa mwaka wa fedha 2020/21 ilikuwa Sh. bilioni 6.6 ila kwa mwaka huu wa fedha 2021/22 bajeti ni Sh. bilioni 16.3," alisema.

Viongozi wateule walioapishwa jana ni Sophia Mjema kuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Jaji Omar Othman Makungu kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania na Jaji Mustapha Siyani kuwa Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania.


**bgtl BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **NMB BANK** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa wadaiwa wanaotajwa hapo chini, walipe madeni wanayodaiwa na benki hiyo pamoja na riba kama inavyooneshwa kwenye notisi za madai tulizowapa Pamoja na ongezeko la riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) zilizodhamini mikopo hiyo kwa **MNADA WA HADHARA.**Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana zilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA | TAWI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | YUSUPH KASIM MBOETO/GOODLUCK ALEX TITO | Nyumba ya makazi iliyopo **Mabibo Sahara** yenye leseni ya makazi **KND/MBB/MBO16/114** Manispaa Ya Ubungo. | 27/10/2021 | ILALA |
| 2 | MARIA OBETH MWASOMOLA | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja na.488 kitalu'S' **Tabata Segerea -Magombani** | 30/10/2021 | ILALA |
| 3 | TENTONE IMAGING TECHNOLOGY/KUMBUKA DEUS NTEJA | Nyumba ambayo haijakamilika iliyopo **Kigogo Kati** yenye leseni ya makazi **KND/KGG/KST11/82** | 27/10/2021 | ILALA |
| 4 | HUSSEIN ISSA SINYALI/PHINAS SAMSON DANIEL | Nyumba ya makazi yenye Hati Ya Mauziano Iliyopo Kisemvule kitongoji cha kitangini | 30/10/2021 | ILALA |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**
**Email: info@bestgoup.co.tz**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**NMB Bank PLC,**
**Ohio Street / Ali Hassan Mwinyi Road,**
**P.O. BOX 9213,**
**DAR ES SALAAM**
**elephone: +255 22 2322550**
**email: Benedicto.Baragomwa@nmbbank.co.tz**

116508502


# CHADEMA yampa masharti 3 Msajili

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demkorasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetoa masharti matatu ili washiriki mkutano ulioitishwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya siasa Oktoba 21 na 22 mwaka huu.

Mojawapo ya masharti hayo ni kutaka kuondolewa kwa zuio la mikutano ya hadhara ambalo vyama vya siasa vimewekewa.

La pili, kutaka Mwenyekiti wa Chama hicho, Freeman Mbowe, aachiwe huru na kuondolewa mashtaka yote yanayomkabili bila masharti yoyote.

Mbowe na wenzake watatu wanakabiliwa na kesi ya ugaidi katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, ambayo inaendelea kusikilizwa.

La tatu, ni kutaka viongozi na wanachama wake wote ambao wako gerezani katika maeneo mbalimbali waliofunguliwa kesi kwenye uchaguzi mkuu mwaka jana waachiwe huru.

Masharti hayo yalitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu Bara wa Chama hicho, Benson Kigaila, wakati akizungumza na waandishi wa habari jana Dar es Salaam kutoa maazimio ya Kamati Kuu ya chama hicho iliyoketi juzi kwa njia ya mtandao.

"Maazimio ya kikao cha Kamati Kuu kilichofanyika jana(juzi) kwa njia ya mtandao ni kwamba pamoja na mambo mengine, kimeamua kwamba CHADEMA hatutashiriki mkutano ulioitishwa baina ya wadau wa vyama vya siasa na Jeshi la Polisi Oktoba 21 na 22 mwaka huu mpaka masharti yaliyoazimiwa na Kamati Kuu yatekelezwe," alisema Kigaila.

"Ili tushiriki ni lazima zuio la mikutano liondolewe, tusiende kama vyama ambavyo vinatoka mahabusu ili vyama vifanye kazi yao kwa mujibu wa sheria. Pia hatutaenda kwenye vikao mpaka Mbowe awe huru ili twende naye kwenye vikao," alisema Kigaila.

"Pia katika magereza mbalimbali hapa nchini, viongozi na wanachama wetu wengi wamejaa huko baada ya uchaguzi mwaka jana, kwa mfano kwa Gereza la Mbozi mkoani Songwe, kuna viongozi na wanachama 40 wako humo zaidi ya miezi 12 sasa na hakuna kinachoendelea, tunataka waachiwe bila masharti."

"Yuko mama mmoja ni mgonjwa ana zaidi ya miezi 12, ukienda Rorya, Simiyu, Mtwara na sehemu nyingine nako watu wetu wako ndani, hatuwezi kwenda kwenye vikao wakati watu wetu wanateswa ndani.'

Pia Kigaila alisema wako tayari kukutana kwa mazungumzo na Rais Samia Suluhu Hassan endapo maombi hayo hayatatekelezwa.

"Tuko tayari kukutana kwa mazungumzo na Rais, lakini hatuko tayari kukutana na Msajili wakati mambo haya hayajatekelezwa, yakitekelezwa tutakutana na yasipotekelezwa tutasubiri kikao na Rais tumwambie mambo ambayo ni muhimu yakatekelezwa," alisema Kigaila.

## HABARI KITAIFA

# Rais Mwinyi aitaka EAC kupitia sera sekta utalii

**Na Allan Isack,** ARUSHA

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezitaka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kufanya mapitio na marekebisho ya kisera za kitaifa katika sekta ya utalii ili kuongeza idadi ya watalii wanaokwenda kutembelea vivutio katika nchi wanachama wa Jumuiya hiyo.

Rais Mwinyi aliyasema hayo jana jijini Arusha, wakati akifunga na kuweka jiwe la msingi la kuanzishwa kwa maonyesho ya utalii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mwenyekiti huyo wa Baraza la Mapinduzi, alitaka nchi za EAC kufanya maboresho na marekebisho kwa nchi hizo zinatofautiana kisera katika sekta ya utalii.

Alisema endapo nchi hizo zitapitia sera hizo na kuanzisha programu mpya katika sekta hiyo zitasaidia kuvutia watalii kwenda kutembelea vivutio vya utalii.

"Tunatakiwa kupitia sera zetu za kitaifa kwa kuanzisha progamu mpya ambazo zitasaidia kuwavutia watalii wengi zaidi kuja kutembelea vivutio vyetu," alisema Rais Mwinyi. Kadhalika alisema kuwa kabla ya ugonjwa wa Covid-19 nchi za Afrika Mashariki katika soko la hisa la Afrika sekta ya utalii ilichangia kwa asilimia 80.6.

Hata hivyo, alisema kwa sasa kuna uhitaji kwa mamlaka husika wa kufanya kazi kubwa ili kuhakikisha wanaongeza idadi ya watalii wanaokwenda kutembelea vivutio vya utalii katika nchi hizo.

Vile vile, alisema maonyesho hayo yatasaidia kufungua utalii wa EAC fursa za kibiashara kwa watalii kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, alisema Julai mwaka huu, alisema mawaziri sita kutoka nchi wanachama walikutana na kufanya kikao na kupitisha namna nchi hizo zitakavyoshirikiana kuutangaza utalii kwa pamoja badala ya kila nchi kufanya peke yake. Alisema baada ya kikao hicho Tanzania, mawaziri hao sita walitoa ridhaa ya kuandaa maonyesho ya utalii ya kwanza ya Afrika Mashariki.

Katika hatua nyingine, Waziri Ndumbaro, alisema kwenye maonyesho hayo wamehudhuria watu zaidi ya 100 kutoka nchi 19 za bara la Afrika na nyingine kutoka nje ya Afrika zikiwamo kutoa mabara ya Ulaya na Asia.

Aidha alisema baada ya kutamatishwa kwa maonyesho hayo, watu hao watakwenda kutembelea vivutio katika hifadhi za Serengeti, Ngorongoro, Mkomazi, Nyerere, Burigi, visiwa vya karafu na marashi Zanzibar, kisiwa cha Mafia na Mlima Kilimanjaro.




Wawakilishi wa Kampeni ya Namthamini, Najma Paul na Vaniladama, kutoka kituo cha EATV, jijini Dar es Salaam, wakiwa na baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Uhuru Mchanganyiko baada ya makabidhiano ya taulo za kike. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCU yafungua dirisha la mwisho udahili wanafunzi

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), imefungua dirisha la mwisho la udahili kwa siku tano kwa ngazi ya shahada ya kwanza kwa programu, ambazo bado zina nafasi katika taasisi za elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2021/22 baada ya wadau kuomba.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari na kufafanua kuwa muda ulioongezwa umeanza Oktoba 11 hadi Oktoba 15, mwaka huu.

Prof. Kihampa alisema udahili katika awamu tatu zilizofunguliwa katika mwaka huu wa masomo kwa vipindi tofauti umekwenda vizuri.

"Tume imepokea maombi kutoka kwa wadau mbalimbali wakiomba muda wa udahili uongezwe, ili kuwapa nafasi wale ambao hawakuweza kudahiliwa au kuomba udahili awamu tatu zilizopita wafanye hivyo.

"Tunaomba taasisi za elimu ya juu zile programu ambazo bado zina nafasi zifunguliwe ili kuruhusu waombaji kuomba. Dirisha hili la awamu ya nne likifungwa hakuna lingine litakalofunguliwa, tunaomba waombaji watumie fursa hii." Alisema Prof. Kihampa.

Alisema utaratibu wa udahili katika awamu hii ya nne ni kwamba ndani ya siku hizo tano zitakuwa ni kwa ajili ya kutuma maombi.

"Kwa siku mbili kuanzia Oktoba 19 vyuo vitatakiwa kutumia kuwasilisha tume majina ya waliodahiliwa, Oktoba 24, vyuo vitatangaza majina ya waliodahiliwa na kuthibitisha udahili kwa walioshindwa kudhibitisha udahili wao katika awamu za udahili zilizopita kutokana na sababu mbalimbali," alisema.

Prof. Kihampa alizitaka taasisi za elimu ya juu, kuzingatia idadi ya wanafunzi iliyoidhinishwa katika programu husika.

# Shule 120 Dar es Salaam sasa kufundishwa historia ya Nyerere

**Na Maulid Mmbaga**

SHULE 120, jijini Dar es Salaam, zimealikwa nyumba ya Makumbusho kuwawezesha wanafunzi kujifunza kivitendo historia ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamishna Mwandamizi wa Uhifadhi Kanda ya Mashariki wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Zainabu Ally, alisema kwa miezi mitatu kampeni hiyo, itazifikia shule zote.

Pia, alisema katika kuelekea kilele cha maadhimisho ya kifo cha Baba wa Taifa yatakayofanyika Oktoba 14, mwaka huu, TANAPA inatoa wito kwa wadau na Watanzania kuungana nao kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, nyumba ya kumbukizi na maeneo mengine yenye vivutio vya utalii.

"TANAPA inapenda kuutaarifu umma juu ya uwapo wa hifadhi ya Taifa ya Nyerere, ambayo ilitokana na sehemu ya lilipokuwa Pori la Akiba Selous, ambalo Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli alilipandisha hadhi na kuwa hifadhi mwaka 2019," alisema na kuongeza;

"Hifadhi ya Nyerere ni ya kwanza kwa ukubwa Tanzania na Afrika pia imebeba jina la muasisi wa taifa letu hivyo inatoa chachu kwa Watanzania wote na kuenzi jitihada kubwa za Mwalimu Nyerere katika uhifadhi wa maliasili na maeneo yake kwa kupenda kutembelea maeneo yaliyohifadhiwa kwa lengo la kujifunza na kupumzika."

Kwa upande wake, Afisa Mwandamizi wa Uhifadhi TANAPA, Seti Mihayo, alisema hifadhini humo kuna fursa mbalimbali za uwekezaji hasa katika upande wa utalii na kuwataka wananchi kuhakikisha wanatembelea hifadhi hiyo, ili kujifunza na kupumzika.

"Zaidi ya asilimia 75 ya watalii wanaofika katika hifadhi nchini, wanatembelea hifadhi ya Nyerere, ambayo ni kubwa kuliko zote nchini na mwitikio wa watu wa ndani kutembelea Makumbusho ni hafifu, hivyo kampeni hii ambayo ilianza Oktoba Mosi, itaendelea hadi Desemba 3, mwaka huu, itaegemea katika kuhamasisha jamii kutembelea hifadhi na nyumba ya kumbukizi, ili kujua uwapo wake na kujifunza historia ya muasisi wa taifa," alisema Mihayo.



TOLEO MAALUM

AUDA-NEPAD
AFRICAN UNION DEVELOPMENT AGENCY

JICA

# MKUTANO WA KILA MWAKA WA AFRIKA KAIZEN -

## Tukio kubwa zaidi la Kimataifa kwa KAIZEN barani Afrika - ulifanyika Dar es Salaam

Mkutano wa 4 wa mwisho wa mwaka wa KAIZEN Afrika (AKAC 2021) ulifanyika katika ukumbi wa Hyatt Regency, Dar es Salaam kuanzia Agosti 24 mpaka 26, 2021. Mkutano uliandaliwa kwa pamoja baina ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA) na Shirika la Kimataifa la Maendeleo Japan (JICA). Mkutano wa AKAC, tangu mwaka 2018, umekuwa ukiandaliwa kila ifikapo mwisho mwa mwaka kama tukio kubwa lenye hadhi ya kimataifa kwa ajili ya KAIZEN Afrika ukiwa na lengo la kubadilishana maarifa na uzoefu baina nchi na kusambaza falsafa za KAIZEN katika bara zima la Afrika. Kwa Tanzania, ilikuwa ni mara yake ya kwanza kuendesha mkutano mkubwa kama huu katika mtindo wa kuchanganya hadhira mbili tofauti (wale wanaoshiriki moja kwa moja na wale wanaoshiriki mtandaoni) hii yote ni kwa sababu ya tishio la ugonjwa wa Uviko-19. Zaidi ya Watanzania 130 walishiriki moja kwa moja ukumbini Hyatt Regency na zaidi ya washiriki 700 kutoka katika nchi zaidi ya nchi 20 walijiunga na mkutano huo kwa njia ya mtandao. Wakati wa mkutano huo, shughuli za KAIZEN za Tanzania zilitambulishwa kwa nchi zingine kwa mfululizo wa vipindi.



*Hybrid Style AKAC (Connected between on-site speakers and participants at Hyatt Regency DSM, and online speakers and participants from more than 20 countries)*





*Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Marehemu William Tate Ole Nasha akizungumza katika ufunguzi wa mkutano huo. Ole Nasha alifariki Septemba 27, 2021. Roho yake ilale mahali pema peponi.*




*Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Zanzibar, Omar Said Shaaban akizungumza katika hafla ya ufungaji wa mkutano huo.*

### Uwasilishaji wa mfano wa KAIZEN Tanzania - kesi ya kwanza ya utekelezaji wa shughuli za KAIZEN kwa upande wa kongano la viwanda

Shughuli za KAIZEN zimetekelezwa katika nchi zaidi ya 10 za Afrika tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000. Kwa Tanzania, Wizara ya Viwanda na Biashara na Jica wamekuwa wakitekeleza kwa pamoja mradi ujulikanao **“Uimarishaji Viwanda vya Kati kupitia Uboreshaji wa Tija na Ubora (KAIZEN),”** tangu mwaka 2013. Tanzania ndiyo nchi ya kwanza kwa Afrika kutekeleza mpango wa KAIZEN kwa kutumia kongano kwa maendeleo ya viwanda. Pia inajulikana kama “Mfumo wa KAIZEN wa Tanzania” na mfumo huo ulitambulishwa kwa nchi zingine za kiafrika katika siku ya pili ya mkutano huo. Mradi huo ulichagua kongano la viwanda vitatu (yaani kongano la viwanda vya zabibu huko Dodoma, kongano la viwanda vya uhandisi chuma mkoani Morogoro, na kongano la viwanda vya mpunga Mbeya) na kundi jingine jipya lililoko Kagera ambaloni kongano la kampuni ndogo zaidi ya 100 ambazo zimechukuliwa kama sehemu ya majaribio na waliweza kutumia mpango wa shughuli za KAIZEN kwa kampuni za kongano hilo mwanzoni mwa mwaka 2020. Kulingana na uwasilishaji, takriban asilimia 70 za kampuni zinazoshiriki zimepata mafanikio makubwa katika upande wa muda wa kuwasilisha bidhaa za wateja kwa wakati muafaka, uokoaji muda wa utafutaji bidhaa, utengenezaji nafasi kupitia shughuli za KAIZEN.




### Majadiliano yaliyokutanisha wajumbe 8 kuhusu uongezaji kasi wa utekelezaji wa mpango wa KAIZEN

Majadiliano hayo yalisimamiwa na Katibu wa Tawala wa zamani wa Mkoa wa Dodoma, Paul Maduka Kessy na kuwasilishwa na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, Dar es Salaam, Dk Edwin P. Mhede na wawasilishaji wengine saba. Washiriki wa majadiliano hayo walijadili kuhusu “Kuongeza kasi ya Maendeleo ya Viwanda kupitia KAIZEN nchini Tanzania”. Wajumbe walihitimisha majadiliano kwa kuangazia umuhimu wa uongozi wa juu, teknolojia, ushiriki wa sekta binafsi, na kutekeleza sera za kuongeza kasi zaidi.

# TOLEO MAALUM




## Kampuni za Kitanzania zilitambulisha KAIZEN

Mabanda ya kampuni mbalimbali kwa ajili ya kutambulisha shughuli zao za KAIZEN Kampuni nne zinazowakilisha kampuni zingine ambazo zinatekeleza shughuli za KAIZEN nchini Tanzania ziliweka mabanda yao huko Hyatt Regency na kuonyesha bidhaa zao wakati wa mkutano wa AKAC. Walitambulisha bidhaa zao na shughuli za KAIZEN kwa washiriki na vyombo vya habari.

| Jina la Kampuni | Biashara | |
|---|---|---|
| AtoZ Textiles Limited | kiwanda cha uzalishaji bidhaa za nguo n.k | -Kiwanda Bora cha Utekelezaji wa shughuli za KAIZEN katika Mkutano wa AKAC uliofanyika Tunisia 2019 |
| KIOO. Limited | Mzalishaji mkubwa wa bidhaa za vioo | -kilishinda kwa kuwa kiwanda bora cha uwakilishi wa viwanda vingine vikubwa vya shughuli za KAIZEN katika tuzo za 2021 na kinaongoza kwa uzalishaji wa chupa kwa Afrika Mashariki |
| CRACODE (*) | Kiwanda kinachozalisha bidhaa asilia na pamba nchini | -kìmeweza kutangazwa kuwa kiwanda bora cha uwakilishi wa viwanda vidogo na kati kwa tuzo za mwaka 2021 |
| Raha Biveradges | mzalishaji wa vinywaji baridi (hususan vile vinavyotokana na ndizi) | -kilipendekezwa kuwania tuzo ya kiwanda bora cha shughuli za KAIZEN 2021<br>-Kilitambulisha shughuli za KAIZEN katika "Ziara ya Kushuhudia Shughuli za Kiwanda Mtandaoni" katika mkutano wa AKAC |
| WOISO Original Products | Wazalishaji wa bidhaa za ngozi | -Wamebeba sifa ya kutekeleza shughuli za KAIZEN kwa miaka kadhaa sasa |

(*) Cultural Crafts Consultants & Designs Co. Ltd



*Kushoto: Kampuni ya AtoZ Textiles Limited / Kulia: KIOO Limited*



*A to Z Textiles Limited: Imetengeneza Barakoa iliyo dariziwa bendera ya Japan na Tanzania*

## Kwa siku zijazo, shughuli za KAIZEN nchini

KAIZEN inamaanisha "Uboreshaji endelevu". Mkutano wa AKAC wa mwaka 2021 ulihitimishwa, lakini falsafa ya KAIZEN bado inaendelea. Wizara ya Viwanda na Biashara imepanga kutekeleza shughuli za KAIZEN kwa wafanyabiashara wapatao 1,500 wa Kitanzania ifikapo mwaka 2030 kulingana na sera yao inayoitwa "Mfumo wa Uboreshaji wa Ubora na Tija (KAIZEN) katika sekta ya viwanda 2020-2030" (FKM 2020-2030). Kwa kuongezea, mwaka ujao wa 2022, Mkutano wa 8 wa Tokyo juu ya Maendeleo ya Afrika (TICAD8) utafanyika Tunisia, na viongozi wa kisiasa (ikiwamo wakuu wa nchi) kutoka nchi za Afrika na Japan watakutana na kubadilishana mawazo juu ya maendeleo ya Afrika. KAIZEN pia itajadiliwa katika mkutano wa TICAD8 kama eneo muhimu kwa viwanda vya Afrika. Inatarajiwa kwamba Tanzania inaweza kupata maendeleo zaidi na kuboresha mpango wake wa KAIZEN kwa nchi zingine za Kiafrika na Japan katika TICAD8 ijayo.

## Namna ya kujifunza KAIZEN kupitia mtandaoni

JICA iliboresha vifaa vya video ambavyo hutumiwa bila malipo ili kujifunza KAIZEN Agosti 2021 na kuzitangaza kupitia mtandao wa YouTube. Uliwekwa utaratibu wa vipindi 3 kama ifuatavyo.
Ikiwa una nia, tafadhali jiunge nasi!







| Kipindi cha 1<br>Kinaangazia mkakati wa uongozi | Kiindi cha 2<br>Auasibu | Kipindi cha 3<br>Ubora wa uwongozi |
|---|---|---|
| | | |

## Namna gani tunaweza kutekeleza mpango wa KAIZEN?

Mpango wa Ruzuku Zaidi ya Wakufunzi 100 wa KAIZEN wamethibitishwa na Wizara ya Viwanda na Biashara nchini, na wanaweza kutoa huduma za ushauri kuhusiana na KAIZEN kwa viwanda na kampuni mbalimbali Huduma hizo ni za kulipia, lakini Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo nchini (SIDO) linatekeleza mpango wa ruzuku kwa ajili ya kupeleka wakufunzi wa KAIZEN katika maeneo lengwa ifikapo tarehe 31 Oktoba, 2021.

| | |
|---|---|
| Kampuni/Viwanda zinazo legwa | 1. viwanda vya uzalishaji katika mikoa 8 ya mradi wa kwanza (*1) au<br>2. washirika wa Kongano kwa mwaka wa fedha 2021/22 (*2) |
| Kipindi | Muda wa maombi wa ushauri kwa shughuli za KAIZEN: 31st October 2021<br>(hitimisho la zoezi zima la ushauri : 31st December 2021) |
| Maelezo | Ruzuku hiyo inajumuisha gharama za usafiri na chakula cha mchana sambamba na gharama za huduma ya ushauri wa KAIZEN unaofikia Sh 50,000 mpaka 60,000 kwa siku tatu (*3) |
| Maswali/Maombi | Contact for SIDO (https://www.sido.go.tz/sw/ofisi-za-sido) |

(*1) Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mwanza, and Singida
(*2) KEKO (Dar es Salaam), KUNAMO (Morogoro), SIMUSOPA (Singida), Mwanza Rice Field Cluster
(*3) The applicant enterprise pays the whole or part of the remaining costs (e.g. remuneration for the KAIZEN Trainer.)

- **KAIZEN ni nini?**
  "KAIZEN" ni neno lenye asili la Kijapani linalomaanisha "Uboreshaji endelevu", na falsafa ya usimamizi na ujuzi wa uendelezaji wa ubora na tija wa taasisi lengwa. Pia ni mkakati uliotanguliza maslahi ya binadamu mbele, unaokuza umoja, mabadiliko ya fikra, kujitegemea, ubunifu, na busara ya kupata mawazo ya wengine katika kutafuta suluhisho la changamoto tunazokabiliana nazo nchini. "Maendeleo ya Viwanda ya kongano" ni njia ambayo inakusudia kuchagiza ajenda ya viwanda kwa kutumia faida ya ukusanyaji pamoja, uwekaji katika makundi kijiografia wa kampuni zenye mahusiano ya moja kwa moja na taasisi washirika katika uwanja eneo fulani. Kuhimiza ushiriki wa nguvu taasisi na kampuni zinazohusika karibu na minyororo ya thamani, na kushawishi ushirikiano kati yao ambao husaidia kukuza ubunifu na viwanda vya ndani.

- **Kuhusu JICA**
  Shirika linalosimamia misaada ya nchi ya Japani (Msaada Rasmi wa Maendeleo). Ni moja wapo ya mashirika makubwa zaidi

- **Kwa Maelezo Zaidi wasisliana na:**
  **Tanzania Kaizen Unit (TKU), Ministry of Industry and Trade (MIT)**
  **P.O.BOX 2996, Dodoma; Tel +255 (026) 2963470**
  **https://www.mit.go.tz/pages/application-forms**

  **Japan International Cooperation Agency (JICA) Tanzania Office**
  **P.O. Box 9450, Dar es Salaam, Tel: 022-211327/30**
  **https://www.jica.go.jp/tanzania/english/index.html**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watumishi wa umma wawe na hofu ya Mungu

**JUZI** Rais Samia Suluhu Hassan aliwaonya watendaji dhidi ya udokozi wa fedha za kampeni ya kitaifa ya miezi tisa ya maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano ya UVIKO-19, huku akisema wanaotaka kuona rangi yake halisi wajaribu kuchezea fedha hizo.

Fedha hizo ni Dola za Marekani bilioni 576 ( Sh. trilioni 1.3) ambazo zitaelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi ya afya, maji na elimu ambayo inagusa maisha ya wananchi moja kwa moja, na lengo ni kuboresha maisha yao na kukuza uchumi wa nchi.

Rais alisema kuna tabia baada ya fedha kupatikana watu wanaunda kamati ambazo huwa ni kichaka cha kujipatia fedha, na kuonya uundwaji wa kamati hizo kuwa kwa umakini kwa kuwa na wataalamu watekelezaji na siyo watu wa kujipatia fedha.

Aidha, aliagiza kila mkoa kuwa na timu ya ufuatiliaji wa miradi husika ambayo moja kwa moja itaulizwa juu ya utekelezaji wake, ili kuepuka kuwa na timu nyingi kwa maana ya ngazi ya mkoa na wilaya.

Rais alitoa kauli hiyo kwa msisitizo kuonyesha ni kwa kiasi gani anakerwa na matumizi mabaya ya fedha za umma, huku fedha nyingi ikielekezwa kwenye kugharamia posho na matumizi mengine na kiduchu ikiwafikia wananchi kupitia miradi ya maendeleo.

Hakuna ubishi kuwa mshirika wa maendeleo yeyote anapotoa fedha anataka kuona zinawafikia wananchi moja kwa moja na kuleta matokeo kwa maana ya kubadilisha maisha yao, lakini imekuwa desturi kuwa sehemu kubwa ya fedha inatumika kugharamia posho, vyakula na gharama nyingine ambazo kimsingi hazigusi maisha ya wengi.

Ni muhimu watendaji wakatanguliza hofu ya Mungu kwanza kabla ya kujinufaisha binafsi na fedha za umma, kwa kuwa wanaowadhulumu ni watu ambao wangeendelea kuishi ikiwa huduma za afya zingeboreshwa kwenye maeneo yao au wangepata elimu na maji kwa manufaa yao na vizazi vijavyo.

Ikiwa mama, mtoto au Mtanzania anapoteza maisha kwa kuwa tu analazimika kusafiri umbali mrefu kupata huduma hizo zimekosekana kwa sababu kuna mtu ametumia mwanya huo kujipatia fedha za kujinufaisha yeye na familia yake, basi kuna tatizo kubwa na inavunja moyo walipakodi.

Ikiwa kila mmoja atakuwa na hofu ya Mungu na kutambua kuwa amepewa dhamana ya kuwatumikia Watanzania, na kila shilingi ikawa na thamani kwa kutekeleza miradi husika, basi mbele ya haki hatakuwa na deni, lakini ikiwa atatanguliza ubinafsi itakuwa ni kuumiza nchi na kujirundikia dhambi.

Zipo nchi zimefikia kiwango cha juu kabisa cha nidhamu ya utumishi wa umma kwamba mtu anaacha kujifikiria mwenyewe bali anawafikiria wananchi, anapopewa jukumu analitekeleza kwa weledi, ustadi, uadilifu na uaminifu mkubwa kwa kuwa anajua ipo siku ataulizwa au nafsi itamuuma sana kuwa hakuwatendea haki wengine.

Kila mwaka ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), inabainisha uwapo wa madudu mengi ambayo yanatokana na usimamizi mbovu wa fedha za umma, na kwa ujumla huonyesha jinsi gani watu wanashindwa kuwajibika, hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma.

Haitarajiwi kuona fedha hizi zinaishia mikononi mwa wajanja wachache bali tuone miradi iliyotekelezwa kwa kiwango cha juu. Tunarajia kuona uzalendo katika kujali Watanzania wengine badala ya ubinafsi wa kujilimbikizia mali.

Fedha hizi na nyingine zinazopokelewa kutoka nje ni mkopo kwa Watanzania ambao watazilipa kwa miaka mingi ijayo, ndiyo maana inatakiwa uaminifu na uwajibikaji wa hali ya juu kuhakikisha zinatekeleza miradi husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Sera kutoa elimu bure inavyomuenzi Nyerere

Na Sabato Kasika

**ALHAMISI** Oktoba 14, Watanzania wataadhimishi kumbukizi ya miaka 22 ya kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Nyerere Rais wa kwanza wa Tanzania, aliyefariki dunia Oktoba 14 mwaka 1999 ikiwa ni miaka 14 tangu ang'atuke kwenye nafasi hiyo ya juu, aliyokuwa anaishikilia tangu kupata uhuru mwaka 1961.

Yapo mengi aliyoyatenda kwa taifa wakati wa uongozi wake ambayo yamemfanya aitwe Baba wa Taifa, ikiwamo kutaka kila Mtanzania apate elimu, kwa kuwa ndiyo msingi wa maendeleo.

Enzi ya uongozi wake, alitoa elimu bure, lakini pia kulikuwapo na madarasa ya elimu ya watu wazima iliyokuwa ikiitwa ngumbaru, kwa wale ambao hawakupitia mfumo rasmi, kuwasaidie wajue kusoma na kuandika.

Ikumbukwe kuwa baada ya uhuru, aliwatangazia vita maadui watatu, ujinga, maradhi na umaskini, hivyo akawekeza zaidi kwenye elimu kwa lengo la kutokomeza ujinga, ili iwe rahisi kumaliza hao wengine wawili.

Kile alichokisimamia kwenye elimu wakati wa uongozi wake, kiliendelezwa na waliochukua nafasi na hata alipofariki dunia waliomfuatia wameendelea kuhakikisha watoto wanapata elimu.

Sasa ni miaka 22 tangu alipofariki dunia, lakini alichosimamia kwenye elimu wakati wa uongozi wake kinaendelea kudumishwa ili kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule asome kadri anavyoweza.

Kwa mfano, sera ya elimu bila malipo ilianza rasmi nchini baada ya serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani mwaka 2015 na bado inaendelea katika awamu ya sita.

Sera hiyo inamaanisha kufutwa kwa ada zote katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne na lakini michango kwa wazazi na walezi katika ngazi ya elimu ya msingi.

Sera hiyo imeleta ahueni kwa wazazi na walezi, hasa kulingana na hali duni za kiuchumi za Watanzania wengi na imekuwa na tija katika sekta ya elimu, kwani imetoa fursa kwa kila mtoto kusoma.

Kumekuwapo na taarifa mbalimbali kuwa, hatua za serikali kutoa elimu bure zimehamasisha watoto wengi kuandikishwa shule kila mwaka, na hicho ndicho Baba wa Taifa alichokikusudia kwamba kila mtoto apate elimu.

Maendeleo hayo ya elimu kwa sasa, mzizi wake ni Mwalimu Nyerere ingawa zipo changamoto kadhaa kwa sasa, kutokana na kutomwandaa mwanafunzi kujitegemea badala yake wahitimu huzunguka kutafuta ajira.

Pamoja na hayo, kusoma ni hatua na kupata ajira ni hatua nyingine, hivyo umuhimu wa elimu uko palepale, iwe ya kujitegemea au kutojitegemea, kwani mtu anaweza kuitumia kufanya mambo makubwa ya maendeleo.

Zipo juhudi mbalimbsli zikifanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa elimu za kutoa mafunzo ya kuwezesha wahitimu watarajiwa kujipanga kwa ajili ya kujiajiri badala ya kutamani kuajiriwa tu.

Ni kweli kwamba, shule nyingi zinakabiliwa na uhaba wa madarasa, madawati, walimu na vifaa vya kufundishia, lakini angalau kile alichokiasi Baba wa Taifa cha kutaka kila mtoto apate elimu kinaendelezwa.

Kwa wale ambao hawakupata elimu katika mfumo rasmi, walipata elimu ya ngumbaru, kwa sasa wamewekewa mfumo mwingine kama Mpango wa Elimu kwa Waliokosa (MEMKWA), ulioanza kutekelezwa na awamu ya tatu.

Vilevile, ili kuhakikisha Watnzania wanapata elimu, kumekuwapo na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ambayo ni programu ya serikali ya kuboresha elimu ya msingi kwa watoto wote nchini.

Hiyo ni programu inayojumuisha wasichana na wavulana, matajiri na maskini, pamoja na watoto wenye ulemavu, ikilenga kuhakikisha hakuna hata mmoja anayeachwa nyuma katika kupata elimu.

Kinachofanyika kwenye elimu leo, kinaakisi kile ambacho kiliasisiwa na Baba wa Taifa, hiyo yanapotajwa mafanikio ya elimu nchini, jina la Hayati Baba wa Taifa, linahusika kwa kiasi kikubwa.

RIPOTI MAALUM

# Madaktari watoa ushuhuda corona

## •Matabibu waliougua wanena

Na Romana Mallya

"ASIKWAMBIE mtu, ugonjwa huu ni hatari! Yaani unaumwa bila kujua utapona au la," Dk. Elisha Osati anakumbuka madhila wanayowapata madaktari baada ya kuambukizwa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa UVIKO-19.

Daktari huyo wa magonjwa ya ndani ikiwamo moyo na mapafu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), anasema licha ya kwamba anatumikia taaluma hiyo, mara zote wao ndio wenyeji wa corona, ana mengi zaidi ya haya.

Dk. Osati ambaye pia ni Rais mstaafu wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), anauogopa ugonjwa huo na ameshuhudia kwa kina madhila yake kutoka kwa wagonjwa wake, ikizingatiwa huduma yake kuu inapatikana walipo wagonjwa mahututi, maarufu ICU.

Kwake unapomtajia maradhi ya corona kuanzia wimbi la kwanza, lilimuumiza na matabibu wenzake, huku kukiwa na hisia za simanzi kutokana na baadhi yao kufariki dunia na yeye akiwa ni miongoni mwa waliougua, akishuhudia awamu ya pili aliyougua, "lakini Mungu ni mwema yakapita hayo".

Si kwamba anashabikia chanjo, bali ni mtetezi mkubwa na alionekana kwenye orodha ya mwanzo kabisa waliokuwa kwenye foleni ya kutaka kuchanjwa mara tu baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuweka wazi utaratibu umeanza nyumbani.

Dk. Osati, ambaye pia ni mtafiti na mhadhiri katika Chuo cha Utafiti na Tiba (MUHAS) anasema Februari mwaka huu baada ya kugundua amepata maambukizi, alijitenga na haikuwa rahisi kwake kwa sababu alilazimika kukaa mbali na mke, watoto na waliomzunguka mpaka alipopona.

Akiwa mwathirika wa janga hilo, anasimulia madhila yaliyompata kwa kusema: "Asikuambie mtu, ugonjwa huu ni hatari! Yaani unaumwa bila kujua utapona au la.

"Halafu kisaikolojia unaathirika zaidi hasa tunaokaa na wagonjwa wakati wote unakuwa unafahamu dalili zote, mawazo ni mengi, unawaza ugonjwa wenyewe, hatua utakazozipitia kipindi cha kuugua kuanzia za awali hadi mwisho."

Daktari huyo ambaye ni mchambuzi wa masuala ya tiba, anasema wakati wa mlipuko wa kwanza wa corona ulioripotiwa nchini Machi 16 mwaka jana, alishuhudia watumishi wenzake walioupata, ambao waliugua na wengine kupoteza maisha.

"Niliona watumishi wenzangu walipata ugonjwa wa corona na wakaugua sana na wengine wakafa, wengi walikuwa ni vijana. Kwa kweli ni hali Fulani, ambayo ni ngumu kidogo, kwa waliougua watanielewa," anasema.

**ATHARI KIUCHUMI**

Dk. Osati anasema unapougua UVIKO-19, mbali ya kupata athari za kiafya, pia unaathirika kiuchumi kwa kulazimika kutumia fedha kupata matibabu badala ya fedha hizo kutumika, kwa ajili ya kuendesha familia.

"Hata kama una bima bado kuna gharama ambazo unaingia au familia itaingia au serikali itaingia. Kwa ujumla gharama ni kubwa kumuhudumia mtu mwenye corona. Ukipata corona alafu ukaanza kukohoa, hewa inabana huwezi kupumua, kichwa kinauma, mwili unauma kwa kweli ni hatua ambayo haielezeki," anasema.

Dk. Osati anapaza sauti watumishi wa kada hiyo iwe ni lazima kukatiwa bima ya afya, akibainisha kuwa bima aliyonayo ni ya kawaida, sawa na watumishi wenzake wengi.

"Sina bima ya maisha, hata wenzangu wengi hawana na kwa bahati mbaya watu bado hawajaielewa bima ya maisha na kampuni za bima hawajajua hilo ni eneo ambalo linatakiwa kuwekeza zaidi kwa kuelimisha na kuhamasisha watu kuzikata," anashauri.



Dk. Elisha Osati

Anasema kutokana na hali waliyopitia na wenzake, wameamua kutafuta namna ya kupata bima ya maisha kwa sababu wanafanya kazi kwenye mazingira yenye hatari nyingi.

"Binafsi ninawaona wagonjwa wa corona na ninafanya kazi kwenye kitengo cha moyo na mapafu na Chumba Maalum cha Wagonjwa wa Uangalizi Maalum (ICU), ambako kuna wagonjwa hao sana.

"Huwa ninawafanyia vipimo vya moyo kadri wanavyokuja, athari ni kubwa. Kuna wenzangu ambao niko nao kwenye idara moja waliugua zaidi, wanatumia oksijeni na gesi hiyo kwa sasa imekuwa shida kidogo, kwa ujumla ni hali ambayo ni ngumu na inaogopesha," anasimulia.

Anakumbuka mwaka jana ugonjwa huo uliporipotiwa nchini kwa mara ya kwanza na kusimulia kuwa baadhi yao baada ya hofu, walipatwa na woga na kukimbia, lakini kadri siku zinavyokwenda wakajifunza zaidi namna ya kujikinga.

**KINGA YA BARAKOA**

Dk. Osati anataja barakoa kama mkombozi mwingine kwao, akisisitiza kuwa imekuwa kinga kubwa kwao na wameona namna ilivyosaidia na maambukizi ya corona.

Wakati mtaalamu huyo akiitaja barakoa, mtaani zinauzwa kati ya Sh. 500 hadi 1,000 kulingana na ubora -- zipo zinazotengenezwa kiwandani na zile za kushonwa mitaani.

"Barakoa na kunawa kila wakati, matumizi ya vitakasa mikono, kwa sababu tunahudumia wagonjwa na mara zote tunakutana nao uso kwa uso, barakoa zimekuwa zikitusaidia kwa kiwango kikubwa," Dk. Osati anasema na kuongeza:

"Katika wimbi la kwanza la corona la mwaka jana, hospitali yetu (Muhimbili) tulikuwa na wafanyakazi zaidi ya 200, waliokuwa wamelazwa kwa wakati mmoja.

"Hata hospitalini ilishindikana ikabidi wakalazwe hospitali za wanafunzi kule Chole Road. Hao wote walikuwa wanaumwa na wanatumia oksijeni," Dk. Osati anasema.

Anasimulia kuwa baadhi yao walipata nafuu na wengine wachache walifariki dunia na katika hilo walijifunza barakoa inasaidia, hivyo kwa sasa wanavaa muda wote wakiwa kazini au katika mazingira yenye mikusanyiko.

**WASIWASI NYUMBANI**

Ili kuzikinga familia zao dhidi ya baa hilo, Dk. Osati anasema anachofanya na matabibu wenzake ni kuhakikisha wakiwa kazini au kwenye mikusanyiko, wanachukua tahadhari zote ikiwa ni pamoja na kujisafisha vizuri kabla ya kurejea nyumbani na kubadilisha nguo na barakoa.

"Kwa sababu ninaona wagonjwa wa corona, lazima nichukue tahadhari zote niwapo kazini, ili niwe salama ninaporejea nyumbani.

"Imekuwa ni utamaduni wangu kila siku ninapomaliza kazi nguo, ambazo nimezivaa ninazivua kazini na kuvaa nyingine. Ninajisafisha vizuri, ninavaa barakoa mpya na kabla ya kuingia kwenye gari, ninahakikisha sanitizer (kitakasa mikono) inahusika, angalau hapo ninakuwa nimeondoa wasiwasi.

"Nyumbani kwangu lazima kunawa, ninahakikisha nguo nilizotoka nazo kazini ninaziweka pembeni na kujisafisha ndipo ninakutana na familia yangu. Utamaduni huu nimejiwekea baada ya athari tulizozipata na wenzangu," Dk. Osati anawasilisha.

**CHANJO YA CORONA**

Dk. Osati anasema baada ya serikali kuridhia chanjo na kuipokea Julai 24 mwaka huu, alikuwa miongoni mwa watu wa awali kuchanjwa.

"Watu wengi siyo kwamba wanapinga chanjo, lakini ni wasiwasi tu kulingana na maneno yaliyotoka kwenye mitandao, kiujumla Watanzania siyo kwamba wanapinga chanjo, wataipokea tu taratibu.

"Ilipoingia nilichanja mapema sana na hii ilinisaidia na imenijengea kujiamini zaidi kuwahudumia wagonjwa, watu wengi wa afya wamechanja, inawezekana kuna baadhi bado wana wasiwasi kidogo kama ilivyo kwa watu wengine.

"Endapo watu wengi watachanja, watatupa kujiamini zaidi, kwa sababu hawajachanja, tunawahudumia kwa tahadhari kubwa kwa kufuata miongozo ya kujikinga na magonjwa ya kuambukiza," anasema.

Anabainisha kuwa wapo watumishi wa sekta ya afya, ambao ni madaktari wamefariki dunia, wamefiwa na ndugu zao na mmoja wao alipofiwa na wanafamilia sita ndani ya wiki moja kutokana na maradhi ya UVIKO-19.

"Madaktari, watumishi wa sekta ya afya ndiyo tunaowahudumia siku zote, tunachowaambia wachanje, sisi tumechanja, chanjo ni salama sana, tumechanja hatujaona madhara yoyote yaliyotutokea, pia tunaelewa kama hujachanja madhara ni makubwa. Corona inaleta madhara makubwa," anasisitiza.

**AJITOSA UTAFITI**

Mtaalam huyo wa afya anasema amelazimika kufanya utafiti wa janga la corona, ili kubaini athari zake.

"Nilikuwa ninafanya utafiti kwenye TB (Kifua Kikuu), moyo na mapafu, lakini kwa sasa kwenye PhD (Shahada ya Uzamivu) utafiti wangu umelenga kuangalia madhara ya muda mrefu ya corona, ambayo mpaka sasa utafiti unaonyesha ni makubwa, utafiti umeonyesha wagonjwa waliopata corona kali wanapata kitu kinaitwa pafu kutengeneza kovu.

Anafafanua zaidi kuwa" Kwa sababu wadudu wanapoingia mwilini kupitia kwenye pua, baadaye kukimbilia kwenye mapafu, mapafu yanakuwa ni uwanja wa mapambano kati ya mdudu na kinga za mwili, mapafu yametengezwa na mifumo midogo midogo inayobeba hewa.

"Baada ya kupata corona inaleta madhara na mtu anakuwa hana uwezo wa kubeba hewa, anabeba kwa kiasi kidogo kwa sababu yameharibika, hivyo yanabeba hewa kwa kiasi kidogo. Tuna wasiwasi pia corona inaweza kuleta madhara kwenye vina vya uzazi."

**RAIS WA MAT**

Rais wa MAT, Dk. Shadrack Mwaibambe, anashuhudia alivyougua corona katika wimbi la pili na kulazimika kujitenga nyumbani kwake kwa muda wa wiki tatu.

"Nilikaa nyumbani kwa muda wa wiki tatu. Bahati nzuri mke wangu ni daktari, akawa ananihudumia. Kuna mambo mengi, ambayo ni sintofahamu.

"Pamoja na kuugua, niliendelea kulala kitanda kimoja na mke wangu, lakini mke wangu hajaugua. "Niliona wanandoa wengi akiwamo... (anamtaja mmoja wa maprofesa na hospitali anayofanyia) aliyeugua corona, akalala wiki tatu na alikuwa anakwenda kuhudumiwa na mke wake, ambaye alikuwa havai barakoa wala glovu, chumba kimoja, mke wake hakuugua."

Dk. Mwaibambe anasema aliugua wakati yuko likizo na muda wa kutakiwa kazini ulipowadia, ilibidi aongeze wiki nyingine nyumbani, ili kuhakikisha hapeleki ugonjwa kwenye eneo lake la kazi.

"Nilipopata corona, kitu kikubwa nilichoondoa na mke wangu ni ile hofu, tulihakikisha hofu haipati nafasi, hivyo tuliendelea na maisha kama kawaida, hii ilitusaidia sana.

"Watu wafahamu kwamba kuna watu asilimia 80, wanaweza kupata corona na wala asiwe na dalili na wengine asilimia 15 wakaugua na kwenda hospitalini, ninajiona nipo miongoni mwa asilimia 15 na mke wangu yawezekana alikuwa miongoni mwa hao asilimia 80, wanaupata lakini wanaendelea na maisha yao.

"Hii ilikuwa mara ya kwanza kwangu kuugua na kulala nyumbani kwa muda mrefu namna hii tangu mwaka 1993, nilipoumwa malaria nikiwa darasa la saba," anafafanua.

**MTIKISIKO WIMBI LA PILI**

Dk. Mwaibambe anasema wimbi la kwanza la corona lililoripotiwa Tanzania Machi 16 mwaka jana, lilisababisha hofu kwa madaktari wengi kutokana na kutokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu ugonjwa wenyewe.

"Kama unakumbuka, dunia nzima ilikuwa na taharuki. Hata pale ulipojaribu kutafuta takwimu mtandaoni hazikuwa nyingi, sehemu kubwa kwa madaktari ilikuwa ni hofu kujua unasambaa kwa njia gani.

"Katika wimbi la kwanza, uvaaji wa madaktari hata wale waliokuwa wanakwenda kuzika waliofariki dunia tulishuhudia maziko yakifanyika usiku, wazikaji walivaa kama mtu anakwenda mwezini, mwili mzima ukiwa umefunikwa.

"Hofu ya namna hii ilichangia watu washindwe kuhudumia wagonjwa, kwa sababu wakati ule tulikuwa hatuna vifaa vya namna hiyo, hivyo ilikuwa huwezi kumgusa mgonjwa."

Dk. Mwaibambe anasema ilipotokea daktari ameingia kwa mgonjwa na kumgusa, hofu iliongezeka zaidi na wengi waliogopa kurudi nyumbani wakihofia kupeleka maambukizi kwenye familia zao.

"Ninakumbuka madaktari wengi walikaa karantini (kujitenga), walikuwa hawaendi nyumbani kukutana na familia zao kwa sababu tu ya hofu ya kumgusa mgonjwa wa corona.

"Wapo wengine walikwenda mbali zaidi, hata viatu walivyokuwa wakivaa waliona walikokanyaga labda wameondoka na mdudu," anasimulia.

Rais huyo anasema kadri elimu ilipotolewa zaidi na wao wakafahamu kuwa wanaweza kuwahudumia wagonjwa kwa kuchukua tahadhari za maambukizi, hofu hiyo ilizidi kupungua.

Tatizo lingine analitaja kuwa, katika wimbi la kwanza la corona, wengi waliamini wagonjwa hao wanatakiwa kuhudumiwa na hospitali kubwa kama Muhimbili, Bugando, KCMC, lakini kadri siku zilivyokwenda, ikabainika hata zile za kawaida wahudumu waliopo huko wanaweza kuwadumia.

ITAENDELEA

# ACT yachambua uchaguzi mdogo

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimetaja baadhi ya changamoto zilizobainika kwenye uchaguzi mdogo uliofanyika maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, alibainisha changamoto tatu kuu ambazo zinatakiwa kutatuliwa kabla ya kwenda kwenye uchaguzi mwingine.

Mojawapo ya changamoto ambayo kimetaja ni pamoja na muda mfupi ambao Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imekuwa ikiuweka kwa ajili ya vyama vinavyoshiriki chaguzi hizo kujinadi kwa wananchi.

Nyingine kimebaini kwamba bado kuna tabia ya Jeshi la Polisi kutumia nguvu kubwa kudhibiti wapinzani kwenye baadhi ya kata zinazofanya chaguzi hizo.

Nyingine bado kuna tabia ya baadhi ya vyama vya siasa ambavyo vinachukua fomu kwa ajili ya kushiriki katika chaguzi hizo, lakini vinaishia njiani.

"Katika chaguzi hizi ndogo tumebaini bado kuna changamoto licha ya kwamba zimepungua kidogo, mojawapo ni mfupi unaopangwa na NEC ambao ni wiki mbili, tatu au usiozidi mwezi mmoja kwa ajili ya kujinadi. Sasa kwa muda huu huwezi kupita kila eneo na kujieleza, muda ni mdogo inabidi hili liangaliwe upya," alisema.

Sababu nyingine ambayo kimeitaja ni kuwapo kwa baadhi ya vyama kutengeneza



mazingira ya kutaka kupita bila kupingwa, huku kikitoa mfano kwenye Jimbo la Ushetu, kwamba vyama vilivyochukua fomu kwa ajili ya kushiriki uchaguzi vilikuwa 16, lakini hatua ya mwisho vilivyofika ni vyama viwili vya ACT- Wazalendo na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Jambo jingine ambalo alisema wamebaini ni kuwapo kwa tabia ya baadhi ya vyama kushindwa kufuata ratiba ya kuendesha kampeni inayokuwa imepangwa na NEC na hivyo kuingilia mikutano ya vyama vingine.

Shaibu alisema pia wamebaini kwamba baadhi ya matokeo yanayotangazwa kwenye baadhi ya maeneo hayaakisi idadi ya wapigakura wa maeneo husika.

Alisema chama hicho kinaamini kwamba suluhisho la changamoto hizo zinazojitokeza ni kufumua sheria ya uchaguzi zilizopo na kuanzisha mchakato mpya wa kufanyia mabadiliko ya kikatiba na kisheria yatakayohakikisha kwamba NEC inakuwa huru na kuiwezesha kufanya kazi kwa haki na ya kuaminika.

"Tunataka NEC ifanye kazi kwa uhuru na kusiwe na makada wa chama cha siasa kama ilivyo sasa ambapo wakurugenzi ambao wanatokana na chama cha siasa ndio hao wanasimamia uchaguzi, tunataka iwe na watendaji wake kuanzia ngazi ya taifa mpaka chini," alisema Shaibu.

Pia alisema imefika wakati sasa kuona namna ya kuanza mchakato wa Katiba mpya baada ya kusubirisha mchakato huo kwa muda mrefu.

Aidha, alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kukutana na vyama vya siasa kwa ajili ya majadiliano.

"Baada ya Rais kukutana na wadau mbalimbali katika kipindi chake hiki ndani ya miezi sita, na ile subira aliyoiomba kwa wadau wa vyama vya siasa, sasa umefika wakati akutane na wadau hawa wa vyama vya siasa," alisema Shaibu.

Kuhusu chama hicho kushiriki katika kikao kilichoitishwa na Ofisi ya Msajili wa vyama hivyo Oktoba 21 na 22, Shaibu alisema bado wanatafakari na watatoa taarifa baada ya kufanya vikao vya ndani.

## Watatu wafariki ajalini akiwamo mstaafu

**Na Waandishi Wetu, SONGEA**

WATU watatu wamefariki dunia akiwamo mstaafu aliyekuwa akienda kuwaaga watumishi wenzake baada ya kustaafu kazi.

Mstaafu huyo aliyekuwa mtunza kumbukumbu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma, ametajwa kuwa ni Devota Challe (60).

Ajali hiyo ilitokea jana baada ya bajaji kugongana na basi la Jeshi la Wananchi katika eneo la Mfaranyaki barabara kuu ya Mbinga -Songea.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Joseph Konyo, amesema tukio hilo lilitokea jana majira ya saa 12:30, asubuhi.

Aliwataja wengine waliofariki katika ajali hiyo kuwa ni Alei Komba, ambaye umri wake haukufahamika, mfanyabiashara mkazi wa Matiri Wilaya ya Mbinga na mwingine anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka (30-35), ambaye hadi sasa hajatambulika ni mkazi wa wapi wala jina, huku dereva wa bajaji hiyo, Alfred Kihwili (Shida) akipata majeraha kichwani na shingoni.

Afande Konyo alifafanua kuwa bajaji hiyo yenye namba za usajili MC580 CYD, ilikuwa ikitokea Luhuwiko ikiwa imebeba abiria hao watatu na ilipofika katika maeneo ya Mfaranyaki basi la Jeshi lililobeba wafanyakazi lilikuwa likielekea Luhuwiko na lilipojaribu kuipita gari lingine likangongana na bajaji hiyo.

Akimzungumzia marehemu Devota, Kamanda huyo alisema alikuwa akienda hospitalini alikokuwa akifanyia kazi kuwaaga watumishi wenzake.

Hata hivyo, mmoja wa ndugu zake ambaye hakupenda kutajwa gazetini, alisema Devota alikuwa anaenda kwenye misa ya shukrani aliyoimba baada ya kustaafu.

Kamanda Konyo alitoa wito kwa madereva wa vyombo vya moto kuwa makini wanapokuwa barabarani hasa madereva wa magari makubwa, ambao wanaongoza kwa kuwasababishia ajali wenye magari madogo, pikipiki na bajaji.

Alisema dereva wa gari hilo la jeshi ambaye alikimbia baada ya ajali anasakwa na polisi.

**Kamanda Konyo alitoa wito kwa madereva wa vyombo vya moto kuwa makini wanapokuwa barabarani hasa madereva wa magari makubwa, ambao wanaongoza kwa kuwasababishia ajali wenye magari madogo, pikipiki na bajaji.**


TANGAZO LA KIFO



DKT. BASIL A. SAPRAPASEN

Familia ya Saprapasen kwa huzuni, tunasikitika kutangaza kifo cha Baba yetu Mpendwa **DKT. BASIL A. SAPRAPASEN** kilichotokea tarehe 07 Oktoba, 2021.

Msiba upo nyumbani kwa Marehemu Kinondoni mkabala na Bank ya Stanbic, Mtaa wa Mafinga, Kinondoni - Dar es Salaam.

Ibada Takatifu itafanyika katika Kanisa la **Mtakatifu IMMACULATA** UpangaDar es Salaam Jumatano, 13 Oktoba, 2021 saa 7:00 Mchana na Mazishi yatafanyika katika makaburi ya Kinondoni Dar es Salaam, saa 9:00 alasiri.

*2Timotheo 4:7*


## Wanusurika kifungo cha miaka 30 jela, waachiwa

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Tanzania imeamuru Maulid Dotto maarufu Mau Mchina na wenzake wawili waliokuwa wanatumikia kifungo cha miaka 30 kwa unyang'anyi wa kutumia silaha na kuiba Sh. 700,000 watolewe gerezani na adhabu ifutwe.

Uamuzi huo ulitolewa na jopo la majaji watatu, Jaji Jacob Mwambegele, Jaji Dk. Mary Levira na Jaji Issa Maige.

Mau Mchina, Nestory Antony maarufu China na Bavona Ernest, walipinga kutiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na Mahakama Kuu kubariki adhabu hiyo walipoipinga mara ya kwanza.

Walalamikaji walishtakiwa kwa unyang'anyi wa kutumia silaha, ilidaiwa Mei 14, 2011 saa 10 alfajiri walivamia nyumbani kwa Abeid Kassim akiwa amelala na mkewe Mwanahamisi Salehe.

Ilidaiwa wavamizi walikuwa na mapanga na mume alijificha juu ya dari na kubaki mkewe ambaye alilazimishwa kutoa Sh. milioni 10 walizotoa benki.

Mke ambaye ni shahidi namba mbili aliwapa Sh. 300,000 na walipofanya upekuzi walifanikiwa kupata Sh. 400,000 na kufanikiwa kuchukua jumla ya Sh. 700,000 na laptop.

Katika usikilizwaji wa rufani, walalamikaji walijiwakilisha wenyewe huku upande wa serikali ambaye ni mlalamikiwa uliwakilishwa na Florida Wenceslaus na Gladness Senya.

Walalamikaji waliomba kuachiwa huru wakidai walifungwa kimakosa kwa sababu ushahidi wa maelezo ya onyo ulitolewa na kupokelewa kimakosa, utaratibu wa kupokea vielelezo haukufatwa.

Wakili wa Serikali, Florida akijibu alidai ushahidi haukuwa na nguvu na haikuwa vyema kuwatia hatiani walalamikaji kwa ushahidi dhaifu wa kimazingira.

Alikubali kwamba kulikuwa na makosa katika upokeaji wa kielelezo cha maelezo ya onyo ya mlalamikaji watatu, pia mashahidi walishindwa kufafanua mwanga ulikuwa kiasi gani wakati wa tukio hilo likitokea.

Katika uamuzi jopo lilikubaliana na hoja za walalamikaji na hoja za upande wa serikali kwamba kielelezo kilipokelewa kimakosa.

Lilisema kwamba utaratibu wa kutoa na kupokea kielelezo haukufuatwa, kielelezo kilipokelewa kwenye kesi ndogo, alitoa shahidi wa nane ambaye alikuwa shahidi wa sita, lakini hakuna kumbukumbu inayoonesha kwanini hakutoka kielelezo hicho akiwa shahidi wa sita.

HABARI KITAIFA

## Zaipuna awapa siri wasichana kufanikiwa

**Na Mwandishi Wetu**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, amefichua siri ya mafanikio yaliyosababisha kuongoza taasisi kubwa ya kifedhe nchini, huku akiwataka wanafunzi kufuata nyayo zake hasa kwa kuzingatia mambo manne.

Akizungumza katika mahafali ya kidato cha nne Shule ya Sekondari ya Wasichana wenye vipaji ya Kilakala mkoani Morogoro, Ruth alisema kuwa mafanikio yanahitaji kumtanguliza Mungu kwa kila jambo na kufanya kazi kwa bidii.

Ruth alisema kuwa uaminifu na uadilifu ndio moja ya nguzo katika jambo lolote alifanyalo mwanadamu iwe katika elimu, kazi majumbani au kuajiriwa, kujiajiri huku akiitaka jamii kufanya yote kwa bidii, uadilifu na uadilifu kwani hiyo ni njia ya mafanikio.

"Nidhamu ni jambo la msingi na muhimu mno hivyo ni nidhamu pekee itayokuwezesha kutawala maisha yako na kuwa na mahusiano bora na wengine lakini kufanya kazi kwa bidii, uaminifu na uadilifu ni silaha nyingine,"alisema Ruth.

Ruth alisema yeye ambaye alisoma shule ya wasichana wenye vipaji ya Kilakala miaka 30 iliyopita na wao kama Benki ya NMB wataendelea kutilia mkazo jukumu lao la uwajibikaji katika jamii katika nyanja mbalimbali ikiwamo eneo ya elimu, afya, majamba yanayoikumba nchi kama mafuriko na vimbunga vinavyoathiri wananchi.

"Sambamba na sera yetu ya uwajibikaji kwa jamii, benki yenu ya NMB inatoa meza 50, viti 50 vyenye thamani ya shilingi milioni 5 pamoja na kompyuta 10 ambazo tuna uhakika zitakuwa chachu ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na pia mazingira ya ufundishaji katika shule hii ya wasichana wenye vijapaji Kilakala,"alisema.

Kwa wanafunzi wa kidato cha nne wanaotarajia kuhitimu mwaka huu, katika risala yao kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB walieleza changamoto zinazoikabili shule hiyo.

Doreen Patrick alisema moja ya changamoto ni pamoja na upungufu wa viti na meza vya kusomea na viti na meza vya bwaloni huku uchakavu wa ukumbi, uharibifu wa milango ya madarasa na mabweni na kukosekana nishati mbadala umeme unapokatika.

Mkuu wa shule hiyo, Mildreda Selula, alisema Shule ya Sekondari Kilakala ina jumla ya wanafunzi 657, huku wanafunzi wanaohitimu wakiwa 88.

Mildreda alisema shule hiyo ina michepuo ya sayansi, biashara na sanaa kwa kidato cha kwanza hadi nne na kidato cha tano na sita kukiwa na tahasusi tatu za sayansi ambazo ni PCM, PCB na CNG na tahasusi moja ya sanaa ambayo ni HGL.

# Serikali yaitaka kampuni Barrick teknolojia upimaji sampuli madini

**Na Faustine Feliciane,**
KAHAMA

SERIKALI imeiagiza Kampuni ya Madini ya Barrick, kuhakikisha inaifikisha teknolojia ya kupima sampuli ya madini kwa mionzi ya X-ray hadi kwa wachimbaji wadogo ili waweze kunufaika nayo.

Kauli hiyo imetolewa jana na Naibu Waziri wa Madini, Profesa Shukrani Manya, wakati akizindua maabara ya kisasa ya kupima kiasi cha madini kwenye mchanga na mawe yanayotoka kwenye machimbo.

Maabara hiyo ya kisasa iliyoagizwa kutoka nchini Australia ni ya kwanza kuwapo barani Afrika.

Profesa Manya, alisema kampuni za Barrick na Twiga zimefanya jambo la maana kuleta mtambo huo na kuzidi kuimarisha uwekezaji uliofanywa na kampuni hiyo katika uchimbaji wa madini ya dhahabu.

"Niwaombe Barrick utaalamu wa maabara hii ya kisasa uwe na faida kwa Watanzania, wapo wachimbaji wadogo wanapata tabu sana kujua uwapo wa madini, ni vyema wakakumbukwa, lakini ujuzi wa kuendesha maabara hii Watanzania nao wapewe kipaumbele," alisema Naibu Waziri Profesa Manya.

Aidha, aliishukuru na kuipongeza Barrick kwa kuteua kampuni ya kitanzania ya ukandarasi ya CSI ya jijini Dar es Salaam kujenga jengo pamoja na kusimika mtambo huo wa kupima sampuli ya madini kwa njia ya mionzi ya umeme (X- Ray).

Kampuni hiyo imetumia miezi saba kufanya tathmini, kuandaa ramani pamoja na ujenzi wa maabara hiyo ya kisasa.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Barrick, Mark Briston, alisema Tanzania ndiyo nchi pekee barani Afrika yenye maabara hiyo.

"Maabara hii itasaidia zaidi katika upimaji wa uhakika, utatumia muda mfupi zaidi, huko nyumba mchakato wa kupima sampuli ulichukua saa nne huku tukitumia kemikali mbalimbali, lakini uwapo wa maabara hii utapunguza muda wa kupima sampuli," alisema na kuongeza:

"Kwa sasa ndani ya dakika mbili tunaweza kupima sampuli na majibu ya kuyapata, lakini hakutakuwa na uchafuzi wa mazingira, mtambo huu haitumii kemikali yoyote."

Kwa mujibu wa Briston, mtambo huo unauwezo wa kupima sampuli 60 mpaka 70 kwa muda wa saa moja pekee.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliomba serikali kujenga kituo cha kodi Mkoa wa Kahama ili kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata huduma ya kodi kwa karibu kuliko sasa.



Mbunge wa Jimbo la Rorya, mkoani Mara, Japhary Chege, akizungumzia mikakati ya maendeleo kwa wananchi wa Rorya wanaoishi Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Marie Stopes yawajengea uwezo wanahabari

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIKA kupanua wigo wa elimu ya afya ya uzazi, Taasisi ya Marie Stopes, imetoa elimu hiyo kwa wanahabari, lengo likiwa ni kuwaongezea ujuzi katika majukumu yao.

Mafunzo hayo yalifanyika mkoani Morogoro na kuwakutanisha wanahabari kutoka vyombo vya serikali na binafsi ikiwamo magazeti, redio na televisheni.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mkufunzi wa masuala ya afya ya uzazi, Dk. Elias Kweyamba ambaye ni daktari bingwa wa magonjwa ya wanawake na uzazi kutoka Taasisi ya Afya ya Ifakara, aliwajengea uwezo wanahabari hao katika maeneo mbalimbali ikiwamo huduma sahihi ya afya ya uzazi wanazotakiwa kupewa wenye wagonjwa.

Kdhalika, Dk. Kweyemba aliwafundisha wanahabari hao sababu zinazosababisha vifo vya kinamama wajawazito na wakati wa kujifungua, akisema miongoni ni kifafa cha mimba, kutokwa na damu nyingi baada ya kujifungua na maambukizi ya bakteria.

Dk. Kweyamba alisema kumekuwapo na vifo vingi vya kinamama na watoto wakati wa kujifungua kunakosababishwa na mambo mbalimbali, lakini vingi vinatokana na sababu za kiafya.

Alisema: "Nimewafundisha afya ya uzazi ili kuunga juhudi za serikali za kupunguza vifo vya kinamama wajawazito na watoto wachanga. Naamini kwa nafasi zao za uandishi wataweza kutoa mchango mkubwa kupitia elimu watakayoitoa kwenye vyombo vyao vya habari."

Kwa upande wake Mkuu wa Mawasiliano wa Marie Stopes, Ester Shedafa, akizungumza katika mafunzo hayo, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuongeza uwezo wanahabari utakaosaidia kutoa taarifa kwa usahihi kuhusu masuala ya afya ya uzazi kwa jamii.

Alisema wanahabari ni kundi muhimu katika kutoa taarifa za afya ya uzazi wa mpango kupitia kazi zao, hivyo wanapaswa kupewa uelewa mkubwa.

Mmoja wa wanahabari waliopata mafunzo hayo kutoka Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Halima Mlacha, alisema mafunzo hayo yamempatia elimu ya kutosha katika kuandika habari za afya ya uzazi na mpango.

Aidha, aliwashukuru Marie Stopes kwa kuwajengea uwezo akisema wamejifunza masuala mbalimbali ikiwamo changamoto wanazokabiliana nazo kinamama wakati wa ujawazito na baada ya kujifungua.

Mlacha alisema: "Nimejifunza namna ya kuripoti habari hizi ili serikali ichukue hatua za kukabiliana na changamoto hizi. Suala la afya ya uzazi bado lina lina changamoto hasa maeneo ya vijijini tuna imani serikali ikiwekeza nguvu kwa kutoa vitendea kazi kwa wakati tutapunguza au kumaliza kabisa tatizo hili."

# Utatuzi migogoro ardhi waleta furaha

**Na Munir Shemweta,** SINGIDA

UAMUZI wa Rais Samia Suluhu Hassan kuitaka timu ya mawaziri wanane inayotembelea mikoa kumi kutoa mrejesho wa utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 kufanya maamuzi bila kuleta taharuki, umeleta furaha kwa wananchi maeneo ya vijiji hivyo.

Timu ya Mawaziri wanane wa wizara za kisekta ikiongozwa na Mwenyekiti wake Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, iko katika ziara ya mikoa kumi kutoa mrejesho wa utekelezaji wa maamuzi ya migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 920 kati ya 975 ambavyo migogoro yake inashughulikiwa.

"Maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ni kufanya maamuzi kuhusiana na migogoro ya matumizi ya ardhi bila kuleta taharuki kwa wananchi na kwa maslahi mapana ya Taifa," alisema Lukuvi wakati wa mikutano na wananchi.

Katika mkoa wa Singida timu ya mawaziri pamoja na wataalamu kutoka wizara za kisekta ilitembelea baadhi ya maeneo ya vijiji 12 vya mkoa mwishoni mwa wiki kujionea hali halisi ya maeneo yenye mgogoro kwa lengo la kujiridhisha na maamuzi yaliyopendekezwa.

Moja ya sehemu waliyotembelea ni kijiji cha Nduamughanga chenye vitongoji vya Mkulu, Nkungi na Majengo Mapya kwenye Kata ya Mughunga Wilaya ya Singida na kubaini sehemu ya vitongoji hivyo yenye ukubwa wa takriban kilomita za mraba 9.645 kuingia ndani ya mipaka ya Pori la Akiba Swagaswaga.

Eneo hilo lina kaya 269 zilizoanzishwa kimakosa kutokana na utata wa tafsiri ya mpaka wa Wilaya ya Chemba na Singida unaopingana na GN ya hifadhi inayoonyesha kuwa hifadhi ipo mkoa wa Dodoma pekee. Mkuu wa Wilaya ya Iramba mkoani Singida, Suleiman Mwenda, alipongeza hatua iliyochukuliwa na Rais Samia kuamuru wananchi wanaoishi vijiji vyenye migogoro ya matumizi ya ardhi kubaki maeneo yao na kuelezea uamuzi huo kuwa utaondoa hofu na taharuki waliyokuwa nayo wananchi kabla ya uamuzi wa serikali.

Mkoa wa Singida una vijiji vyenye migogoro ya mipaka na hifadhi ambapo katika utekelezaji maamuzi ya Baraza la Mawaziri iliamuliwa vijiji hivyo vibaki na mipaka yake irejewe kwa njia shirikishi.

Vijiji hivyo ni Mlandala na Msosa vilivyopo Wilaya ya Ikungi pamoja na vijiji vya Masimba, Mseko, Kizonzo, Nselembwe na Wembere vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba. Eneo la vijiji hivyo ni ardhi oevu yenye vitalu vya uwindaji wa kitalii ambapo wananchi kutoka mikoa ya Singida, Shinyanga pamoja na Tabora wamevamia ardhi oevu ya Wembele kwa ajili ya malisho na kilimo katika eneo hilo chepechepe la bonde la Wembele.

Bonde la Wembele ni chanzo cha maji ya Mto Wembele na mtiririko wa maji ya Ziwa Eyasi na Kitangiri. Eneo hilo ni muhimu kwa ajili ya mapito na mazalia ya wanyamapori na makazi ya ndege hai ambao wako hatarini kutoweka duniani.

Baadhi ya wananchi wakiwamo wabunge wameelezea uamuzi wa Rais kama njia ya kuleta suluhu ya migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya vijiji ambayo wananchi wake wamekuwa wakiishi kwa wasiwasi bila kujua hatma yao.

Mmoja wa wananchi anayeishi kwenye jamii ya wafugaji aliyejitambulisha kwa jina la Iddy Selemani, alisema, kwa sasa ana uhakika maeneo yao yatapangwa upya na kubainisha maeneo ya wafugaji na wakulima na hivyo kutoa muafaka wa matumizi ya ardhi katika maeneo yao.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kondoa mkoa wa Dodoma, Mohamed Huseni Kova, alipokea uamuzi wa Rais Samia kuwabakisha ama kumega sehemu ya maeneo ya hifadhi kwa ajili ya wananchi kwa furaha na kuelezea kuwa ni uamuzi mzuri uliolenga kuwaonea huruma wakulima na wafugaji.

"Ongezeko la watu linafanya kuwe na uhitaji mkubwa wa ardhi na uamuzi wa kuwabakisha wananchi unatoa huruma kwa kuwa kulikuwa na vijana wa maliasili waliotoa adhabu kali kwa wananchi walioingia maeneo ya hifadhi," alisema Kova.



Mkuu wa Kampuni ya Puma Energy Afrika, Fadi Mitri (katikati), akikata utepe kuzindua vilainishi vipya vya Puma kwa ajili ya magari, viwanda na mitambo mbalimbali, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy Tanzania, Dominic Dhanah na Meneja wa Vilainishi vya Puma, Prosper Kasenegala. PICHA: JOHN BADI

# Chanjo magonjwa ya wanyama kuzalishwa nchini

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inatarajia kuanza kuzalisha chanjo za magonjwa ya wanyama ikiwamo ya kichaa cha mbwa katika kiwanda kilichojengwa wilayani Kibaha, mkoani Pwani.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Uvuvi, Profesa Hezron Nonga, alisema wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa.

Prof. Nonga alisema, kiwanda hicho kinatarajia kuanza rasmi uzalishaji wa chanjo hizo Desemba, mwaka huu na zitauzwa kwa gharama nafuu kwa wananchi hususani wafugaji.

"Zipo chanjo za wanyama za kutosha kwenye maduka ya kampuni binafsi ingawa bezi zake ni kuanzia Sh. 2,000, lakini zitakazozalishwa na kiwanda cha serikali zinauzwa kwa gharama ndogo ya Sh. 500 lengo ni kuwezesha wafugaji wengi kuchanja mbwa wao na paka ili kutokomeza ugonjwa wa kichaa cha mbwa," alisema Profesa Nonga.

Alisema kuanza kuzalishwa kwa chanjo hizo nchini kutawezesha serikali kuokoa fedha nyingi zinazotumika kuangiza nje ya nchi.

"Lengo la kiwanda hicho ni kuzalisha chanjo na kufanya biashara ili kuhakikisha wanyama wetu wanapata chanjo na magonjwa ya kichaa cha mbwa yanadhibitiwa," alisema Prof. Nonga.

Alisema hatua hiyo ni miongoni mwa mkakati wa pamoja uliowekwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) ya kutokomeza ugonjwa wa kichaa cha mbwa ifikapo mwaka 2030.

Alisema, wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inachukua hatua mbalimbali za jinsi ya kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa kichaa cha mbwa kwa kutoa elimu kwa wananchi na kuwasisitizia watoto kuacha kuwachokoza, kuwapiga mbwa wanaopita, wanaokula au wenye watoto.

Katika kutekeleza mkakati huo, alisema takwimu za chanjo kwa mbwa na paka kuanzia Julai 2021 hadi Septemba 2021, walifikia 81,345.

Profesa Nonga alisema, takwimu zilizopo kwenye wizara hiyo Tanzania ina mbwa milioni 4.5 na paka milioni mbili wanaofungwa kwa malengo mbalimbali ikiwamo na ulinzi, kusaidia kuchunga mifugo na uwindaji.

Mtaalamu wa afya ya jamii kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Jubilate Bernard, alisema, kati ya Januari hadi Agosti mwaka huu, watu 39,787 walitolewa taarifa ya kung'atwa na mbwa au wanyama wa jamii hiyo.

# BOA kuimarisha zaidi huduma zake

**Na Mwandishi Wetu**

BANK of Africa (BOA) imeeleza dhamira yake ya kuimarisha huduma zake zaidi kwendana na mahitaji ya wateja wake.

Akizungumza katika kilele cha Wiki ya Huduma kwa Wateja, Mkurugenzi Mtendaji wa BOA Africa, Adam Mihayo, alisema:

"Huduma kwa wateja inabaki kuwa eneo kuu la kuzingatia katika shughuli zetu za kila siku kama benki kupitia kauli mbiu yetu ya mwaka huu ya 'Nguvu ya Huduma', benki imeanza kufanya maboresho zaidi ambayo yatanufaisha wateja sambamba na kufanikisha kuleta maendeleo ya nchi."

Alisema hivi sasa wateja wanaendelea kufurahia huduma za benki kupitia matawi yake yaliyopo mikoa mbalimbali nchini na njia nyinginezo mbadala za utumiaji teknolojia ya kidigitali kupata huduma za kibenki ikiwamo matumizi ya mifumo ya BOA Pay inayowawezesha wateja kufanya malipo na makusanyo wakiwa katika maeneo yao ya kazi au wakiwa nyumbani.

Mapema mwaka huu Bank of Africa iliwekwa kuwa miongoni mwa benki 15 zinazoongoza barani Afrika, ikiwa na mtaji wa dola bilioni 2.5, "Tunaamin hatua hii kubwa isingeweza kutimizwa bila wateja wetu, hivyo tunaahidi kuendelea kuwahudumia kwa bidi, hii ikiwa kipaumbele cha msingi katika biashara yetu," alisema Mihayo.

# TBL Plc yang'ara tuzo ya Rais ya Mzalishaji Bora

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia Tanzania (TBL) imetambuliwa kwa kutoa mchango katika kukuza uchumi wa Tanzania kupitia sekta ya uzalishaji, huku ikitangazwa kuwa mshindi wa pili wa tuzo ya Rais ya Mzalishaji Bora wa Mwaka (PMAYA).

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam katika hafla ya kutunuku tuzo za wazalishaji bora.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alikuwa mgeni rasmi katika hafla ya mwaka huu.

Mashindano ya Tuzo ya Rais ya Mzalishaji Bora wa mwaka (PMAYA) hufanyika kila mwaka na Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI) kutambua biashara bora katika tasnia mbalimbali. Tuzo hizo zilitolewa kwa mara ya kwanza mnamo 2005 na zimekuwa zikifanyika kila mwaka. Tuzo hizo zinalenga kutambua na kuthamini jukumu muhimu la sekta ya viwanda katika maendeleo ya uchumi wa Tanzania.

Mkurugenzi wa wa TBL, Jose Moran, akizungumzia ushindi wa mwaka huu alisema, "Ni heshima kutambuliwa kwa mara nyingine tena kwa kuwa mzalishaji bora licha ya kwamba mwaka ulikuwa na mazingira magumu ya uendeshaji biashara. Tunajivunia jinsi mtazamo wetu juu ya ujumuishaji wa kifedha, mipango ya kilimo na huduma za ubunifu zimeboresha maisha ya wengi na kusaidia ukuaji wa uchumi kwa faida pana ya nchi. "

Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa hivi karibuni ya EY iliyopewa jina la Uchambuzi wa Athari za Kiuchumi ya TBL, thamani ya jumla iliyoongezwa na TBL kwa uchumi wa Tanzania ni Sh. bilioni 613 au asilimia 0.5 ya Pato la Taifa, na kwamba asilimia 74 (Sh. bilioni 130 ) ya malighafi inayotumia TBL kila mwaka hupatikana ndani ya nchi.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 12, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

**Kinababa walivyo muhimu kuwaepushia mabinti mimba**





Ukurasa 14

Mzee Mwakangale; alianza shule ukoloni, digrii miaka 10 ya Nyerere

ELIMU

**NA PETER ORWA**

MIAKA 22 BILA NYERERE;

# Namna alivyokokotoa elimu tangu zama Tanganyika hadi kung'atuka

• UPE kung'ara' Afrika; wasomi, JKT; robo ya bajeti elimu

UKIMCHAMBUA mara tu baada ya kupata nafasi ya uongozi wa nchi, Waziri Mkuu wa Tanganyika na baada ya mwaka mmoja Rais, Baba wa Taifa Julius Nyerere, hajawahi kuwa mbali na fani yake ya ualimu.

Baada tu ya kukalia kiti, mpango wake wa kwanza wa muda mfupi wa maendeleo wa miaka mitatu hadi 1964, kati ya aliyoyapa kipaumbele ni elimu. Mara baada ya Uhuru wa Tanganyika, alifuta elimu ya matabaka, ambapo jamii ya kizungu walipewa nafasi kubwa, kufuatiwa na Waasia kisha Waafrika, ikawa sawa kwa wote.

Mzizi wa shule za sekondari kihistoria, nyingi zilizotoka mikononi mwa ukoloni, zikibeba ishara za matabaka, mathalan jijini Dar es Salaam kuna shule kama St. Xavier ambayo leo ni Kibasila; St Francis, leo ni Pugu na hata iliyokuwa Forodhani .

Pia, shule kama hizo za kihisitoria za wasichana jijini, zimo Jangwani, Zanaki na Kisutu, huku za wavulana ni Tambaza na Azania.

Nje ya jiji kuna shule kama Minaki (Kisarawe), Ihungo na Nyakato (Kagera), Mazengo (Dodoma), Mzumbe (Morogoro), Galanos (Tanga), Alliance (Musoma Sekondari) na Malangali (Iringa).

### UWEKEZAJI RASMI

Mwaka 1964, Tanzania ikiwa rasmi katika mfumo wa Muungano, Nyerere aliwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye elimu na kudumu daima kama dira ya maendeleo ya kitaifa hadi sasa.

Mpango huo wa kwanza wa miaka mitano 1964 - 1969, dhima ilikuwa ni kuwatoa Watanzania katika mfumo tegemezi. Mwalimu Nyerere, aliamini elimu ingewafikisha katika ukombozi kamili.

Kwa kipindi cha miaka mitatu ya baada ya uhuru, watoto wa Kitanzania hawakupata elimu ya msingi, ama kwa kukosa nafasi kutokana na nafasi chache au kutokana na upeo duni wa haja ya kutumia nafasi hiyo. Hivyo, mpango ulilenga kupatikana shule kwa wastani kila kijiji, ikizingatiwa asilimia 90 ya Watanzania walioishi vijijini.

Ili kufanikisha hilo, mbinu iliyotumika ni falsafa ya kijamaa, iliyokuwa ni itikadi ya nchi, Tanzania ikiwa na chama kimoja tangu 1964, wananchi walishirikishwa kwenye ujenzi, kama ilivyo katika ujenzi wa sekondari za kata unaoendelea sasa.

Ndani ya mpango huo wa miaka mitano, hadi kutimu mwaka 1967, msukumo mkubwa ulitoka katika Azimio la Arusha, uliofikiwa na chama tawala TANU kikiipa tafsiri 'Namna ya kipekee ya kuufanikisha Ujamaa."

Mwaka 1966, uongozi wa Mwalimu Nyerere, uliona haja ya vijana nchini kuishiriki mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kisheria kwa wahitimu wa kidato cha nne na kupata mafunzo zaidi ya mwaka mmoja au zaidi, kupata vijana bora wa kutumikia taifa kwa moyo, imani na stadi sahihi.



Mwalimu Julius Nyerere, katika moja ya mahafali ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam – Morogoro (sasa SUA). **PICHA: MTANDAO**

Sio kwamba ilipitia salama, bali ilipata mabishano kwa baadhi ya vijana kutokukubali, lakini ilitekelezeka kisheria kwa maana ya kuunda mwelekeo wa kujenga kitaifa. Ni wakati ambao Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kilishaanza,

Hadi hatua ya miaka 10 ya Uhuru, ambayo Mwalimu Nyerere alijisifu kuwapo maendeleo makubwa baada ya Tanzania huru, ulikuwa umeshapita mwaka mmoja kuanza Mpango wa Maendeleo wa Pili kitaifa, 1969 hadi 1974.

Tangu kupatikana uhuru wa nchi, eneo mojawapo lilibainika kuwa na pengo ni wataalamu.

Rais Nyerere, alitumia mbinu ya Serikali ya Tanganyika na baadaye Tanzania kujenga urafiki na nchi zingine zilizopiga hatua, zikiwapatia vijana nchini, fursa kwenda kusoma Ughaibuni.

Mfano hai ni wataalamu wa uhasibu kwenda kujifunza uhasibu (kama CPA), Associated Chartered Certified Accountancy (ACCA) na Associated Certified Accountancy (ACA), Uingereza, madaktari na fani nyinginezo nchini Cuba, China na iliyokuwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Urusi (USSR); askari na wanahabari na katika vyuo vikuu vya Sandhurst na Cardiff, Uingereza.

### YA AZIMIO MUSOMA

Ndani na mpango huo wa pili, 1969 hadi 1974, mengi yalishuhudiwa katika sekta ya elimu, ambayo Mwalimu Nyerere katika uongozi wake wa TANU na serikali aliundia dira na msukumo.

Ilifika kipindi elimu iliwekewa mapinduzi makubwa, ikiwamo kuchukua hisa kubwa zaidi katika bajeti ya nchi, kuna wakati aliitengea asilimia 20 hadi 25 ya bajeti yote.

Mwaka 1974, Mwalimu Nyerere kupitia kofia yake ya uwenyekiti wa TANU akawezesha kupitishwa mpango, ambao mantiki yake ya kina, una wajihi wa kuendeleza Azimio la Arusha la mwaka 1967.

Hapo kuliundiwa tamko; Azimio la Musoma, lililohimiza kuboresha elimu kwa wote. Ndani pameshuhudiwa mengi kuhakikisha shule za msingi kila kijiji, wazo lililoanza katika mpango wa kwanza, 1964.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA BEATRICE MOSES

# Kinababa walivyo muhimu kuepusha mimba

Ni wazi kuwa taarifa za kupatikana kwa mimba huwa ni njema zaidi kwa wanandoa, huongeza furaha, lakini zaweza kuwa tofauti kwa upande wa wazazi ambao bado hawajaozesha hasa wenye binti ambaye ni mwanafunzi, husababisha mzozo kwenye familia na kuharibu mwelekeo mzuri wa kukamilika kwa ndoto za msichana.

Kuna mila na desturi zimechangia wasichana kukosa elimu ya kudhibiti mihemko yao, kama kutokubali kwenda kukutana na vijana wa kiume mafichoni au kutotembea msichana peke yake maeneo yenye ukimya hatarishi, hivyo mikasa ya kutisha iliyowapata baadhi yao imeripotiwa kwenye vyombo kadhaa vya habari.

Mshauri mwezeshaji wa masuala ya kijamii na afya Rose Kasoga, anasema katika baadhi ya familia taarifa hizo zimezua mzozo na kusababisha amani kupotea kwa kuwa wazazi wa binti husika huanza kutupiana lawama na kinamama hupata lawama za moja kwa moja, huku hatima ya maisha ya msichana husika ikiwekwa rehani

Nafasi ya baba kumsaidia binti kuepuka mimba za utotoni, anasema kuwa baba ana nafasi kubwa kwenye malezi ya familia kwa kuwa ni mtu mwenye mamlaka makubwa yaani kiongozi wa familia, hivyo atahakikisha analinda familia yake wakiwamo watoto wa kike na wa kiume.

"Kinababa wana uwezo mkubwa wa kusaidia binti zao wasipate mimba kwa kuwa wanaweza kuwajenga vyema kisaikolojia kwa kuwapa ushauri mzuri wa kujitambua kuwa thamani ya urembo wao itaongezeka pale watakapothamini elimu, kwamba uhusiano wa mapenzi unahitaji wakati wake," anasema.

Kasoga anasema kuwa kwa sababu baba naye ni mwanaume, hivyo ana uwezo wa kutambua mbinu kadhaa tofauti ikiwamo ulaghai na ubakaji wanazotumia wanaume au vijana wa kiume, anaweza kumsaidia binti yake kuepuka mtego au pia kumuonya kijana wake wa kiume kutowalaghai au kubaka wasichana akimjuza madhara yake.

"Binafsi niliwahi kupata barua ya mtu ananitongoza niliogopa kumwonyesha mama kwa kuwa alikuwa ni mkali na mwenye msimamo, niliificha ile barua na kumwonyesha baba kwa sababu alikuwa ni rafiki yangu na alinisaidia kuvuka kile kikwazo," anasema.

Kasoga anasema baba anayejitambua anajenga urafiki na binti yake ili kumsaidia kuondoa uoga wa kumweleza matatizo yanayomkabili, tofauti na baba yule aliyejengewa imani ya kuwa karibu na bibi, shangazi na mama ndiyo watu anaopaswa kuwaeleza yanayomsibu.

"Baba akiwa rafiki anashiriki kuhakikisha watoto wake wanakula vizuri wanashiba kwa kuwa wapo wasichana waliodanganyika kwa sababu ya njaa, chips na mayai ambavyo vinatajwa kuwa ni miongoni mwa vyakula vinavyosababisha wasichana wengi kunasa je kwa nini isiwe ni sehemu ya mlo kwenye familia," anasema.



Binti mwenye umri ndogo akiwa mjamzito. **PICHA: MAKTABA**

> Umuhimu wa kuamua na kupanga pamoja lini wanaweza kupata ujauzito na idadi ya watoto, endapo wanaume watashirikishwa kama wadau, walengwa na mabalozi wa kuunga juhudi za serikali kupunguza mimba za utotoni.

### ATHARI MIMBA UTOTONI

Taarifa kuwa mwanafunzi hasa wa shule ya msingi au sekondari kupata mimba huwa ni mbaya hata kwa walimu na serikali kwa kuwa hulazimika kumfukuza mwanafunzi mjamzito kwa kuwa huaminika kuwa tayari ameyajua mambo makubwa hivyo 'atawaambukiza' wasichana wenzake.

Jambo hili lilizua mtafaruku mkubwa na baadhi ya mashirika ya kimataifa yakainyoonyea kidole Tanzania kutokana na msimamo uliowekwa na Serikali ya awamu ya tano chini ya Hayati John Magufuli ambaye aliapa kuisimamia kipindi chote cha awamu yake kutoruhusu wasichana waliopata mimba kurejea masomoni.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako alikuwa akisoma Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 bungeni mjini Dodoma, alibainisha kuwa suala ambalo limezungumzwa sana na wabunge na kwa hisia kubwa linahusu wasichana wanapata ujauzito wanapokuwa shuleni.

"Nimesimama hapa nikiwa kama mama, kama mzazi na kama waziri mwenye dhamana ya elimu, hili suala ukitazama michango ambayo imetolewa ni ambalo kwa kweli inabidi tuliangalie vizuri, wizara yangu kwanza inasikitika sana inapoona watoto wa kike wanakatisha ndoto zao za elimu kutokana na sababu yoyote ile ikiwamo ya mimba," anasema Profesa Ndalichako.

"Ninafahamu kwamba mimba kabla ya ndoa inaathiri sana hata kisaikolojia kwa sababu unakuwa kama vile hata ukubaliki na kadhalika. Kwa hiyo, kunakuwa na madhara makubwa ambayo yanakuwa yanajitokeza," anasema.

Anatoa takwimu, za kitabu cha elimu Basic Education Statistics cha mwaka 2016 zilizoonyesha kwamba katika mwaka 2015, wanafunzi wa kike ambao waliacha shule ya msingi kwa ajili ya ujauzito walikuwa 251, na watoto wa kike walioacha shule kwa sababu ya kupata ujauzito walikuwa 37,658.

Mwakilishi Mkazi Mwandamizi wa Shirika la Kimataifa la Pathfinder, Joseph Komwihangiro, anabainisha kuwa mimba za utotoni ni moja ya changamoto inayoikwaza Tanzania katika kufikia malengo yake ya uboreshaji wa huduma za afya ya uzazi kwa mama na mtoto.

Komwihangiro anabainisha kuwa idadi ya wasichana wanaopata mimba katika umri mdogo imezidi kuongezeka kutoka 116 hadi 132, mwaka 2010 hadi 2015/16 (TDHS) na kusababisha Tanzania kuwa nchi ya 17 Afrika yenye idadi ya juu ya mimba na uzazi wa mabinti wanaopevuka.

Anabainisha kuwa umuhimu wa ushiriki wa wanaume katika uboreshaji wa afya ya uzazi unatokana na matokeo ya Kongamano la Kitaifa la Watu na Maendeleo (ICDP) lililofanyika Cairo, Misri ambalo lilisisitiza juhudi za kuwashirikisha wanaume katika masuala ya afya ya uzazi.

Nguvu waliyonayo wanaume katika ushawishi wa maamuzi juu ya afya ya uzazi kwa vijana wa kike ikiwamo uwezo wao wa kuamua wajiingize katika vitendo vya ngono salama na pia kutumia njia za kuzuia mimba.

"Umuhimu wa kuamua na kupanga pamoja lini wanaweza kupata ujauzito na idadi ya watoto, endapo wanaume watashirikishwa kama wadau, walengwa na mabalozi wa kuunga juhudi za serikali kupunguza mimba za utotoni," anasema.

Wanaume wana uwezo wa kuelimishana mwenyewe juu ya madhara yatokanayo na mimba za utotoni kwa kuzingatia miongozo na sheria ya nchi, pia wanaweza kuwaelimisha vijana wa kike na wakiume umuhimu wa matumizi ya njia za afya ya uzazi.

Komwihangiro anaitaja njia hiyo kuwa inaweza kupunguza ongezeko la mimba za utotoni kwa wasichana, pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na mimba za utotoni na kuwawezesha wasichana kumaliza masomo na kupata uwezo wa kujishughulisha na shughuli za uchumi na kuchangia maendeleo ya nchi.

### VISABABISHI MIMBA

Ofisa Mtendaji wa Shirika la Gladers linalojihusisha na uwezeshaji wa kimaendeleo, Damas Kambadu, anasema utafiti mbalimbali uliofanywa unaonyesha kuwa zipo changamoto nyingi wasichana na wanawake wanakutana nazo katika jamii wanazoishi ikiwamo ndoa na familia zenye migogoro, miundombinu mibovu ya afya na unyayasaji wa kijinsia

Kutokana na utafiti uliofanywa na Gladers katika Tarafa ya Miyuji na Mnadani kata za Dodoma kwa mwaka 2020 na 2021, zinaonyesha kuwa mzizi halisi wa matatizo haya yote ni umaskini, hali inayosababisha mabinti waliokwama kumaliza shule kutojihusisha na shughuli zozote za kujitafutia kipato.

Pia, baadhi ya familia kinababa kuwa walevi wa kupindukia na wazembe katika suala la kusimamia familia zao na kuachia majukumu yote kufanywa na wake zao, hali ambayo husababisha mabinti kukosa pesa za mahitaji yao na kujiingiza katika vitendo vya ngono bila hata kutumia kinga kutokana na kuahidiwa kulipwa fedha zaidi.

Anabainisha kuwa baadhi ya wasichana wamejikuta na maambukizi mbalimbali ya magonjwa ikiwamo virusi vinavyosababisha UKIMWI na kupata mimba za utotoni.

"Kutokana na mila za makabila tofauti tofauti ya Tanzania mwanamke anachukuliwa kama mtu mwenye majukumu ya kuzaa na kufanya shughuli za nyumbani, huku mwanamume akipewa ruhusa ya kumiliki mali na mwanamke kunyimwa haki hiyo, jambo linalosababisha mwanamke kuwa na mzigo mkubwa pale ambapo baba wa familia anakuwa ni mlevi na mzembe," anasema.

Kambadu anasema kupitia mradi wa Fahari ya Binti aliyefanikiwa (FABA), Shirika la Gladers liliamua kuwasaidia wasichana na wanawake walioathiriwa na kupata mimba wangali na umri mdogo na kukatishwa kutimiza ndoto zao lilisajili wanafunzi 50, kati ya umri wa miaka 13 mpaka 37, asilimia 60 wanalea watoto hao bila baba.

Anasema asilimia 40 wanaotoka kwenye familia za kimasikini, wanawapa mafunzo ya kiujasiriamali, ikiwamo utengenezaji wa batiki na sabuni na gharama zote za mafunzo hayo zikigharamiwa na Gladers.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, Juni mwaka huu alibainisha mpango wa serikali wa kuhakikisha wanafunzi waliokatisha masomo kwa sababu ya kupata mimba wanarejea shuleni kupitia vyuo vya maendeleo ya wananchi.

Akwilapo akabainisha kuwa hatua hiyo ya kurejesha masomoni wanafunzi hao inatokana na makubaliano ya majadiliano ya muda mrefu baina ya wizara hiyo na Benki ya Dunia na kuwaagiza wakuu wa vyuo hivyo kutekeleza hatua hiyo chini ya Mpango wa elimu hauna mwisho kwa kuanza kuwadahili wanafunzi ifikapo mwaka 2022.

Pia, aliagiza vyuo vyote vya maendeleo ya wananachi viwe vimesajiliwa kama vituo vya kufanyia mitihani ya kidato cha pili na kidato cha nne ili kufanikisha kuanza hatua ya kutekelezwa kwa mpango huo unaoweza kuwa chanzo cha nuru mpya kwenye maisha ya mabinti hao.

Mipango ya serikali na mashirika binafsi katika kuwarejeshea mwendo wa hatua za maendeleo mabinti hao zinapaswa kuungwa mkono na jamii, hata hivyo kina baba bado wana nafasi kuwa ya kusaidia kupunguza idadi ya wasichana wanaokatiza masomo kwa kupata mimba wakichukua hatua za kuwasaidia mabinti zao kushinda mitego na vishawishi.



# Namna alivyokokotoa elimu tangu zama Tanganyika hadi kung'atuka

INATOKA UK.11

Ni azimio lenye ajenda 'Elimu kwa Wote' ambayo ina dhima kutoka Umoja wa Mataifa (UPE – Universal Primary Education) , kuunganishwa na upatikanaji elimu kwa walioikosa, chini ya walimu wa kujitolea, kuwezesha wasiopata fursa, kujua kusoma na kuandika chini ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

Ni zama ambapo umma ulionekana kuhamasika hasa wanavijiji kujenga madarasa ya shule mpya vijijini, huku Taifa liking'ara, barani Afrika kupiga hatua kwenye elimu katikati ya miaka 1970, ikiwamo wengi kujua kusoma na kuandika.

Azimio la Musoma utekelezaji wake uliendana na kuanzishwa Vijiji vya Ujamaa vilivyoasisiwa, baadhi ya maeneo walilazimika kuhama na kukawapo mipango ya maboresho; ujenzi wa shule za msingi, mkakati ambao Mwalimu Nyerere alikuwa muumini mkubwa.

Kuasisiwa UPE, ulikumbana na shida uhaba wa walimu. Hapo ikaamuliwa wahitimu bora wa elimu ya msingi, walinolewa vyuoni wakatumiwa darasani, hata wakatoa mazao kwa mafanikio makubwa, licha ya baadhi kukejeli kisiasa, UPE ni 'Ualimu Pasipo Elimu.'

Msukumo wa Azimio la Musoma kutoka kwenye chama, ulizaa pia ajenda ya wahitimu wa kiume waliotoka mafunzoni JKT kwa mujibu wa sheria, kufanya kazi miaka miwili kwanza kabla ya kwenda vyuoni, ilhali dada zao hawakunaswa na kikwazo hicho. Baadaye, uamuzi uliboreshwa, wahitimu wa sayansi nao hawakuguswa.

Hivyo, kisheria kujiunga na masomo zaidi, mbali na sifa za kitaaluma, mlengwa alipaswa kuhudhuria mafunzo ya JKT na kufanya kazi miaka miwili.

Kimsingi mafunzo ya JKT ni sehemu ya alama inayojitegemea kwa tija ya kumboresha kijana wa Kitanzania inayodumu hadi sasa.

### TASISI ZA ELIMU

Pengo la wataalamu takriban kila sekta lilifanyiwa kazi kwa kuanzishiwa chuo maalum. Rais Nyerere aliliona mapema, kwani baada kupitisha Mpango wa Kwanza wa Maendeleo, mwaka 1965, aliunda Chuo cha Maendeleo Mzumbe (IDM) kupata wataalamu viongozi na wa biashara, alianzisha Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na ndani ya msimu huo ndio UDSM iliposajili wanafunzi wake wa kwanza.

Mwaka 1972, ilipitishwa sharia ya kuundwa Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA), ili kupata mamlaka za kitaifa kukidhi uhaba wa wahasibu, ambao awali walisomea nje ya nchi. Ndani ya mwaka huo, pia kilianzishwa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM).

Kilichokuwa Chuo cha Ualimu Chang'ombe, ambacho sasa ni Shule ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DUCE) ni sehemu ya mikakati hiyo.

Mwaka 1973, mwaka mmoja kabla kutangazwa Azimio la Musoma, ilipitishwa sheria ya kuundwa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), huku mwaka 1974, azimio lilihimza maudhui ya Kitanzania. Hadi mwaka 1976, mtaala ulikuwa mezani.

Mwalimu Nyerere, kupitia kitabu chake cha 'Ujamaa Essays' ambacho kinaendana na Azimio la Arusha, alibuni nadharia ya 'Elimu ya Kujitegemea' iliyobeba maana kadhaa.

Inajumuisha maana: Kila hatua ya elimu iwe inajitegemea na isitafsiriwa mtu kafeli, mathalan darasa la saba au kidato cha nne; elimu aipatayo kijana wa Kitanzania ifanane na maisha yake halisi na usomi wake usimfanye atake kazi za ofisini pekee na daima msomi asijitenge na jamii inayomhusu.

### KUONGEZA SEKONDARI

Kutokana na hali halisi baada ya uhuru, Mwalimu Nyerere aliweka jitihada zaidi katika elimu hasa ngazi ya msingi, ili Watanzania wote wafikiwe na waliokosa wakawekewa huduma yao ya madarasa ya jioni maarufu 'UPE' kama ilivyo MMEKWA ya sasa.

Kuna ukweli, kuwa kulikuwapo pengo la wanaojiunga na sekondari. Baadhi ya shule za msingi zilishindwa kuvusha hata mwanafunzi mmoja kujiunga na sekondari. Ndio maana iliwekwa tafsiri 'mwanafunzi hajachaguliwa' na si 'hajafaulu' kujiunga na sekondari.

Nafasi katika sekondari binafsi zilikuwa za kuhesabu na 'academy' za msingi hazikuwapo. Jijini Dar es Salaam kulikuwapo sekondari nane, tatu za wavulana na wasichana kila moja na mbili mchanganyiko.

Hadi mwaka 1976 shule nne binfasi za sekondari za Dar es Salaam, zilikuwa Kinondoni, Vituka Ufundi, Aga Khan Mzizima na Shaban Robert.

Katika jitihada za kuziba pengo, Mwalimu Nyerere, muongo mmoja kabla hajaondoka madarakani, aliwezesha kujengwa sekondari zenye mkondo mahsusi wa kilimo, ambazo ni Ruvu, Kilosa, Kibiti na Ifakara, ambazo zinafanana hata majengo kwa msaada wa serikali rafiki ya Cuba.

Kitaifa, juhudi za kuziba pengo katika elimu ya sekondari ilianzia kwa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) iliyoamua kuunga mkono juhudi za Mwalimu Nyerere kwa kuanzisha sekondari binafsi, zinazojumuisha: Kinondoni (Dar es Salaam), Jumuiya (Tanga), Jitengeni (Same) na Kibohehe (Moshi).

Mwaka 1976, Jumuiya ya Wazazi ya TANU (TAPA) iliungana na BAKWATA, ikaanzisha sekondari nyingi za mikondo ya ufundi na kilimo, baadhi yake ni: Vituka (Dar es Salaam), Lupata (Tukuyu), Boza (Pangani), Bagamoyo Technical (Pwani), na baadaye mwaka mmoja kabla ya kung'atuka Mwalimu Nyerere, ilianzisha shule kama ya Meta ya jijini Mbeya.

Katika sera ya jitihada ya kupanua elimu ya sekondari binafsi, chini ya uongozi wa Rais Nyerere, kukawapo mpango wa kupanua elimu kwa sekondari binafsi, kutokana na msukumo wa mahitaji, kuendana na hali halisi.

Mwanzoni mwa miaka ya 1980, serikali ya Mwalimu Nyerere iliuambia umma wahitaji wa sekondari, kujenga na kisha kufika serikalini kuazima wakuu wa shule na hata walimu wanaopewa mkataba maalum wa ruhusa (secondment), pale wanapompata aliye tayari.

Baadhi ya wakazi waliyochagamkia fursa hizo, ambazo ni mithili ya sekondari za kata za sasa, inajumuisha Njombe (wakati huo ikiwa Iringa) na Wilaya Rungwe.

Njombe waliungana kuanzisha shule kama Mpechi na Mtwango, huku Rungwe walichangamkia fursa kuanzisha shule walizotumia majengo ya zamani na madhehebu ya dini kuwa wadhamini wa shule hizo za wananchi.

Upanuzi wa majengo ulitumia nguvu za wananchi katika mfumo wa harakati za umma kupanua majengo ya shule za msingi, kata zikipeana majukumu mbalimbali.

Mfano hai wilayani Rungwe, kuanzia mwaka 1982 kulishuhudiwa kuanzishwa Shule ya Sekondari Mwakaleli, chini ya udhamini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Dayosisi ya Konde na ilimuazima mwenyeji wa eneo hilo, Andalalalisye Mwaihabi, kutokea Chuo cha Ualimu Tabora, alikokuwa mkuu.

Nyingine ni sekondari ya Lutengano, chini ya Kanisa la Moravian, mwaka 1982; mwaka uliofuata ikaazishwa shule ya Ndembela ikidhaminiwa na Kanisa la Sabato na 1984 shule ya Kipoke, chini ya dhehebu la Baptisti. Ni hali iliyovusha idadi ya sekondari kutoka mbili za awali wilayani humo, moja ikiwa ya serikali - Rungwe.

Wiki hii Watanzania akikumbuka miaka 22 bila ya Baba wa Taifa, ameacha alama kwa kuwa alikuwa 'mwalimu wa kudumu' ikiakisiwa na maisha bifsi, yakiwamo ya uandishi wa vitabu na mashairi.

Hata alipostaafu aliacha mezani ndoto ya mpango wa upanuzi wa vyuo vikuu nchini, ishara kuu aliyobahatika kuishuhudia ni Chuo Kikuu Huria (OUT).

**• Kesho, usikose simulizi zaidi maisha ya Baba wa Taifa kisiasa.**

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Mwakangale; alianza shule enzi za ukoloni, digrii miaka 10 ya Nyerere

• Bibi mwanafunzi wa 1962 ana yake

MWALIMU Julius Nyerere, Rais wa Kwanza wa Tanzania, leo ni miaka 22 tangu kifo chake kilichotokea nchini Uingereza, anakumbukwa mengi hasa katika juhudi za kufuta ujinga, kupigana na adui maradhi, umaskini.

Wakati nchi inapata uhuru, ilirithi mfumo wa elimu kutoka kwa mkoloni, ambao darasa la kwanza hadi la nne; la tano hadi la nane; kisha sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

Ni mfumo uliotumika kwa nchi za Afrika Mashariki, zilizokuwa chini ya koloni la Waingereza, huku shule kadhaa zikiwa za seminari yaani za wamishonari.

Marais waasisi wa nchi tatu, Uganda, Tanganyika na Kenya, Milton Obote, Nyerere na Jomo Kenyatta, walihakikisha elimu hususan ya juu, inaimarika na kuwafikia wananchi wao kwa kukubaliana masuala kadhaa.

Mzee Stephen Mwakangale, mmoja wa walioipata elimu ya mfumo huo, ambaye ana simulizi ya kina katika faragha yake na Nipashe, akisema alianza katika umri utawala wa ukoloni nchini, akaushuhudia uhuru wa Tanganyika akiwa mwanafuzi, Muungano na hata akamaliza chuo kikuu katika miaka 10 ya uhuru.

Hapo anaanza simulizi yake, kwa kupongeza kilichofikiwa sasa kielimu, ikiwamo ongezeko la shule hadi vyuo vikuu, licha ya kutaja vikwazo kadhaa kwa wahitimu wa sasa, hasa kwenye suala la ajira.

Mzee huyo wa leo, mtoto wa mwanasiasa kindakindaki na gwiji wa chama TANU, anakumbuuka alivyosoma, akitamka kwamba: "Kutembea umbali mrefu kufuata masomo au kukaa mbali na wazazi wako tangu ukiwa shule ya msingi ilikuwa si jambo geni. Shule zaidi zilikuwa za bweni.

Ni simulizi inayokumbusha msomi, mwanasiasa na waziri mstaafu, Dk. Juma Ngansongwa, aliyewahi kuwaambia wanahabari, mara yake ya kwanza kuvaa viatu ni pale alipochaguliwa kujiunga na sekondari ya Mzumbe, ikisha sharti la lazima.

Mzee Mwakangale anaendelea: "Nimesoma bweni tangu msingi kutokana na majukumu ya baba yangu alikuwa mtumishi wa umma na hakukaa eneo moja.

"Nilipomaliza kidato cha sita Minaki Sekondari, nilikwenda Chuo Kikuu Nairobi. Kipindi hicho, hakukuwa na chuo kikuu nchini. Tulipangiwa Watanzania 10, kwenda University of London, Campus of Nairobi, Kenya," anasimulia.



Stephen Mwakangale (watatu kutoka kushoto), akiwa na wanafunzi wenzake wa kidato cha sita, Shule ya Sekondari Minaki, Kisarawe mwaka 1967. **NA MPIGAPICHA WETU**

> "Nilikuwa makini kusikiliza kengele ya kanisa Katoliki au adhana. Majira ya mchana, hapo nakuwa nimebaini saa saba mchana imetimia.

Anafafanua ni chuo kilichowakutanisha wana - Afrika Mashariki 30 pekee katika mwaka wa masomo aliyojiunga, huku kila nchi ikitoa wanafunzi 10 kutoa fursa sawa kwa nchi nyingine zilizokosa chuo, tegemeo lilikuwa Chuo cha Nairobi.

"Kuendesha chuo kikuu gharama ni kubwa na nchi hizi zilikuwa zote zimetoka kuwa makoloni. Hivyo, walikubaliana elimu ya juu itakuwa Nairobi, chuo ambacho kilisimamiwa na Waingereza, mitihani ilitoka London.

"Ilikuwa si rahisi kuwapo mitihani feki au elimu feki wakati huo. Juhudi zako zilikuwa ndio msingi. Kwanza, umepata fursa kati ya wengi nchi tatu, wakati huo kabla ya kuhitimu utapokea barua ya kazi utafanyia wapi.

"Nilipohitimu chuo mwaka 1971 nilipangiwa kufanya kazi NBC (Benki ya Taifa ya Biashara) kwa sababu nilichukua shahada 'Bachelor of Commerce'na wengine na fani walipangiwa maeneo tofauti ya kazi," anasimulia, mstaafu akiwa nyumbani kwake, Forest jijini Mbeya.

Anadai ubora wa elimu kutoka vyuo ulifanana na anaendelea: "Suala la vyeti feki lilikuwa hakuna. Chuoni unapokwenda unalipiwa na serikali ila ukishapata ajira unalipa sehemu ya uzalendo ilikuwa mikopo kusaidia gharama za uendeshaji vyuo na wengine wanufaike," anasimulia.

**VYUO VIKUU EACA**

Anasema baada ya uhuru, nchi tatu za Afrika Mashariki zilikubaliana kuendesha vyuo vyao na kugawana aina ya kozi, ili kutoa fursa kwa wananchi wasome fani tofauti.

Stephen Mwakangale, kijana wa zama hizo na babu wa leo, anasema baada ya hapo kukawapo mabadiliko ya hatua za maendeleo. Kila nchi ilisimamia chuo chake, Makerere (Uganda) na Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM) kwa Tanzania, Kenya ikiendelea na Nairobi College, chini ya Chuo Kikuu cha London.

"Campus (kampasi) zilikuwa tatu, Kenya, Uganda, Tanzania pamoja Zanzibar. Nchi zilishirikiana kuendesha vyuo," anasimulia Mwangale na kuendelea:

"Mgawanyo ulikuwa Makerere maalumu kwa Tiba na Elimu (ualimu); UDSM ilijikita kwenye Sheria; Nairobi kwa kuwa ni chuo kilichoanza muda mrefu kiliimarisha kwa kozi nyingi, Uhandisi, Veterinary Science (tiba ya mifugo), Uandishi wa Habari na B.Com (Bachelor in Commerce)."

**SHULE ALIYOSOMA ZAMANI**

Mkazi wa jijini Mbeya tangu mwaka 1962, Grace Mwankusye, anaisimulia Nipashe alivyosoma katika iliyoitwa Government School (Sasa Majengo Shule ya Msingi), akikiri elimu sasa inapanuka kwa ongezeko la shule.

"Elimu yetu ya tofauti na sasa. Nafikiri kutokana na mazingira ya wakati huo, vitu vingi havikuwapo, usafiri, umeme, uchache wa shule ilifanya tutembee umbali mrefu kwa miguu.

"Mimi niliishi Majengo na nilikuwa nasoma darasa la tano 'middle school' ilipo sasa Meta Sekondari. Ili uwahi shuleni, unaangalia jua, kusikiliza adhana au kengele za kanisani," anasimulia.

Anaendelea: "Kwa sababu nyumbani kwetu saa haikuwapo. Kwa hiyo, nitaamka alfajiri nifanye usafi, hadi 1:00 niwe shuleni. Ikifika mchana saa sita unatembea haraka kurudi nyumbani kula chakula.

"Wakati mwingine unakuta mama hayupo nyumbani, itanipasa nikoke kuni, nipike haraka kabla ya saa saba mchana nirudi tena shuleni.

"Nilikuwa makini kusikiliza kengele ya kanisa Katoliki au adhana. Majira ya mchana, hapo nakuwa nimebaini saa saba mchana imetimia."

Grace anasema alipohitimu darasa la nane, hakuchaguliwa kuendelea na sekondari, akikumbuka fursa zao kielimu zilikuwa katika sekondari za Mbeya Day na Iyunga.

"Shule zilikuwa chache ukifaulu unapangiwa hata mkoa mwingine. Kama hukufaulu darasa la nne, mzazi akiwa na uwezo utakwenda shule zilizomilikiwa na Wahindi, Aghakan (sasa Azimio) na Market Primary School sasa hivi Sisimba Shule ya Msingi.

"Kwa ujumla mji ulikuwa kimya kipindi tunasoma miaka ya 1962 hadi 1967. Mji katika makazi yalikuwa kimya, magari hakuna, unaweza kutembea kutoka nyumbani hadi shuleni usikutane na gari hata moja, au ukikutana na gari labda la serikali, au yaliyopaki uhindini. Yaani ilikuwa nadra hata kuusikia mlio wa gari.

"Umeme ulikuwa upo hospitalini, uhindini maeneo machache. Matumizi ya taa za 'chemli' yalikuwa kwenye nyumba nyingi, ila taa za karabai zilitumiwa na familia zilizojiweza kiuchumi kwa sababu ziliuzwa ghali na zenye mwanga mkubwa," anasema Grace.

***•Keshokutwa, usikose kuhusu simulizi rafiki wa karibu Mwalimu Julius Nyerere, marehemu John Mwakangale.***



# Waandishi wa habari waelezwa wajibu wao

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAANDISHI wa habari wametakiwa kutumia kalamu zao kwa lengo la kuisaidia nchi na kujiepusha taarifa ambazo zinaashiria kuchochea migogoro na kuvuruga amani.

Mwenyekiti wa jumuiya ya maridhiano mkoa wa Dodoma, Mchungaji, Dk. Evance Chande, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Dk. Chande alisema Watanzania wanategemea kuona taarifa zinazoleta maendeleo ya nchi badala ya zile zisizo na tija kwa jamii ambazo zinaashiria uchochezi na uvunjifu wa amani.

Alisema kuwa taaluma ya waandishi wa habari inathaminiwa na kuaminiwa na Watanzania, kupitia taarifa zake zinazotolewa kama vile za maendeleo zinazowagusa watu wote bila kujali itikadi yoyote.

"Ni mategemeo ya wengi waandishi wa habari kuandika habari zilizo sahihi ambazo siyo za kuhamasisha na kuleta migogoro na uvunjifu wa amani iliyopo," alisema.

Alisema Watanzania wanategemea kusikia na kuona habari zinazoandikwa zinasaidia serikali na jamii kuleta maendeleo kutokana na mchango mkubwa unaoletwa na waandishi kupitia kalamu zao.

Aidha, aliwaomba waandishi wa habari kuhakikisha wanatumia taaluma yao kufichua maovu kwa lengo ya kuisaidia serikali na jamiii ambayo mara nyingi yamekuwa yakirudisha nyuma maendeleo.

"Bado kuna changamoto kwa baadhi ya vyombo vya habari vimekuwa vinaficha taarifa zinazodumaza maendeleo kutokana na uwapo wa rushwa na kuwafanya hata baadhi ya waandishi wa habari kujikuta wakishindwa kuandika baada ya kupatiwa hiyo rushwa," alisema.

**"Ni mategemeo ya wengi waandishi wa habari kuandika habari zilizo sahihi ambazo siyo za kuhamasisha na kuleta migogoro na uvunjifu wa amani iliyopo," alisema.**

# Mambo saba ya Tanzania mkutano UN wa tabianchi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI ya Tanzania imetaja mambo saba itakayoyatoa kwenye majadiliano ya Mkutano wa 26 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2021/22 serikali itatumia takribani Sh. bilioni 362 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo aliyasema hayo alipokuwa akitoa tamko la serikali kuhusu mkutano majadiliano utakaofanyika mwaka huu nchini Scotland kuanzia Oktoba 31 hadi Novemba 12, mwaka huu.

Waziri Jafo alisema Tanzania itashiriki kikamilifu katika majadiliano hayo yenye maslahi mapana kwa taifa na itaweka msimamo katika mambo mbalimbali ikiwamo rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mkataba na makubaliano ya Paris ambapo kwa mujibu wa Mkataba huu, nchi zilizoendelea ziliahidi kutoa Dola za Marekani bilioni 100 kila mwaka ifikapo mwaka 2025 ili fedha hizo ziwezeshe nchi zinazoendelea kama Tanzania kuweka mipango na mikakati ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Msimamo wa Tanzania katika suala hili ni kuzitaka nchi zinazoendelea kutimiza wajibu wao wa ahadi ya kutoa fedha hizi kama tulivyokubaliana," alisema.

Alitaja jambo la pili ni kujenga uwezo wa nchi zinazoendelea kama Tanzania ili kujiimarisha kwa ufanisi katika kukabiliana na athari zinazohitaji kujengewa uwezo katika kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Mkataba na Makubaliano ya Paris. "Msimamo wa Tanzania katika suala hili ni kuzitaka nchi zilizoendelea pamoja na mashirika ya kimataifa kutilia mkazo suala la kujenga uwezo wa nchi zinazoendelea ili ziweze kutoa mchango wake katika kupunguza uzalishaji wa gesi joto duniani," alisema.

Aidha, alisema msimamo kwenye kilimo na mabadiliko ya tabianchi ambako kumekuwa maoni kinzani kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea kuhusu kujumuisha sekta ya kilimo katika sekta zinazotakiwa kupunguza uzalishaji wa gesi joto.

"Msimamo wa Tanzania ni kuwa, sekta ya kilimo isijumuishwe katika sekta zinazotakiwa kupunguza gesi joto kwa kuwa kilimo kinaathirika sana na athari za mabadiliko ya tabianchi kutokana na kutegemea mvua," alisema.

Kadhalika, alisema msimamo mwingine ni uendelezaji na usambazaji wa teknolojia ambapo msimamo wa Tanzania katika suala hilo ni kwamba nchi zilizoendelea zihakikishe nchi zinazoendelea zinapatiwa teknolojia hizo kwa gharama nafuu na kwa uwazi. Pia alisema msimamo mwingine ni katika mchango wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambapo msimamo wa Tanzania katika suala hilo ni mkutano huo ufikie maamuzi yatakayowezesha upatikanaji wa fedha za kuwezesha nchi zinazoendelea kutekeleza michango yao na mapitio ya michango hiyo yafanyike kila baada ya miaka mitano.

Waziri Jafo alisema msimamo mwingine ni upunguzaji gesijoto kwa kutumia biashara Tanzania imeweka msimamo kwamba nchi inayouza ziada ya upunguzaji isijumuishe kiwango kilichouzwa kwenye orodha yake ya upunguzaji ili kusitokee kuhesabiwa mara mbili kwa kuwa nchi iliyonunua ziada hiyo ndiyo itaweka kiwango hicho kwenye orodha yake ya upunguzaji gesijoto.

Msimamo mwingine ni jinsia na mabadiliko ya tabianchi ambapo Tanzania inahimiza utekelezaji wa programu ya miaka mitano kuhusu jinsia na mabadiliko ya tabianchi.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo (kulia), akizungumza wakati wa kutoa tamko la serikali jijini Dodoma jana, kuhusu ushiriki wa nchi katika mkutano wa kimataifa wa mabadiliko ya tabia nchi utakaofanyika nchini Uingereza mwisho wa mwezi huu, kushoto ni Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega. **PICHA: IBRAHIM JOSPEH**

# 'Tafsiri potofu ya jando na unyago shida'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa mila ya jando na unyago ni nzuri isipokuwa pale ambapo mafundisho yanayotolewa yanakwenda kinyume cha maadili.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Dk. Jerome Kamwela, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumzia hali ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) kwa mtazamo wa kijinsia na baadhi ya mila hatarishi.

Alisema mila hiyo inahamasisha vijana kuanza mapenzi katika umri mdogo bila hata kuwa wameandaliwa kwa namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU.

"Hii ni mila ya jadi ambayo hutumika kumwingiza binti wa kike au kijana wa kiume katika majukumu ya utu uzima," alisema.

Alibainisha kuwa madhara mengine ya mila hiyo ni pamoja na mimba na ndoa za ututoni na pia huhusisha masuala ya tohara ambayo pia huongeza athari za maambukizi ya VVU. Akizungumzia mikakati ya kukabiliana na maambukizi ya VVU, Dk. Kamwela alisema ni pamoja na kujenga uwezo wa wadau kutoa elimu kwa jamii ili kutatua kero za kijinsia katika mwitikio wa VVU na Ukimwi.

"Mwingine ni serikali na wadau wasaidie kuongeza rasilimali fedha kwa ajili ya kusaidia afua zinazosaidia masuala ya wasichana balehe katika mwitikio,"alisema.

Aidha, alisema kuimarisha utendaji wa kamati za kitaifa za kuratibu wadau katika ngazi za kisera na programu ili kuwezeshwa uingizwaji wa mambo ya kijinsia kwenye mwitikio huo.

Hata hivyo, alisema kuendeleza juhudi za kuhakikisha kwamba masuala ya jinsia na VVU yanapewa uzito stahili kwenye Sera ya Taifa ya Jinsia, Mpango Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) na NAIA ili kuhakikisha uunganishwaji wa afua za VVU, afya ya uzazi na ukatili wa kijinsia.

"Kuhamasisha wanaume na wavulana kuwa watetezi na mabalozi katika ngazi zote katika kuhakikisha kuna usawa wa kijinsia na kuondoa ukatili wa kijinsia, kuendelea kuchambua na kubainisha mila na desturi hatarishi zinazobagua wanawake kwenye maeneo mbalimbali na jamii ili kutafutiwa suluhisho," alisema.



# Vituo mafuta vyahamasishwa ujenzi miundombinu gesi asilia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeanza mchakato wa kuhamasisha vituo vyote vya mafuta zaidi ya 1,000 nchini kujenga miundombinu ya gesi asilia.

Imesema lengo ni kuokoa gharama za matumizi kwa wamiliki wa vituo na vyombo vya usafiri.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Meneja Mawasiliano na Uhusiano EWURA, Titus Kaguo, wakati wa semina kwa waandishi wa habari wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Mbeya, Rukwa, Songwe, Katavi, Njombe na Ruvuma.

Alisema serikali imejipanga kuhamasisha matumizi ya gesi asilia inayochimbwa Mtwara na Songosongo ambapo gesi inatumika kwenye viwanda, na kwamba jumla ya nyumba 300 za mkoani Mtwara zimeunganishwa na gesi hiyo.

Kitu ambacho serikali inakifanya kwa sasa ni kuhamasisha matumizi ya gesi kwenye magari na vituo vya mafuta kwa sasa, kuna vituo viwili ambapo kimoja tayari kinatoa huduma za gesi asilia," alisema Kaguo.

Aliongeza kuwa hadi sasa jumla ya magari 300 yameunganishwa na mfumo wa gesi asilia na kwamba lengo ni kuhakikisha magari yote yanaunganishwa kwenye mfumo huo ili kupunguza gharama uendeshaji na kuhimiza matumizi ya nishati mbadala.

Mmoja wa wanahabari, Emmanuel Lengwa, aliiomba EWURA kusimamia bei elekezi za mafuta kwa maelezo kuwa kumekuwa na udanganyifu kwenye vituo vya mafuta.

Alisema kuna udanganyifu unaofanyika kwenye vituo vya mafuta kwa sababu fedha anayotoa mteja ni tofauti na kiasi cha mafuta kinachopatikana.

Meneja wa Mamlaka hiyo Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Karim Ally, aliwaomba wanahabari kutoa ushirikiano kwa mamlaka hiyo ili kuboresha huduma za nishati na maji.

Alisema EWURA wanasimamia taasisi mbalimbali, hivyo aliziomba mamlaka zinazofanya kazi pamoja kuhakikisha wanatoa huduma ipasavyo.




Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, akikata utepe kuashiria ufunguzi wa Duka la Vodashop jijini Mbeya ikiwa ni maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja. Ufunguzi wa duka hilo ni moja ya mikakati kuhakikisha inaleta huduma karibu na wateja wake. Kulia ni Mkurugenzi wa Biashara wa Vodacom Linda Riwa, Mkuu wa Mauzo wa Kampuni hiyo Nyanda za Juu Kusini, Ezekiel Nungwi na kushoto ni Diwani wa Kata ya Sisimba, Josephine Qamunga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wakerwa utitiri wa vyama vya wafanyakazi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya viongozi wa vyama vya wafanyakazi wameiomba serikali kufanya marekebisho ya sheria ili kupunguza idadi ya vyama vya wafanyakazi nchini.

Wamesema kuwa wingi wa vyama hivyo haviwasaidii wafanyakazi kutetea maslahi yao badala yake unazidi kuwadidimiza.

Viongozi wa vyama vya wafanyakazi, walitoa kauli hiyo wakizungumza na Kaimu Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri nchini, Pendo Berege, alipotembelea Chuo cha Wafanyakazi (OTTU), kilichoko jijini Mbeya.

Rose Lamosai, mwakilishi wa TUGHE Mkoa alisema ni muhimu wafanyakazi kuungana kuimarisha chama kimoja ambacho kitatetea maslahi yao kuliko kugawanyika na kuanzisha migogoro.

"Wingi wa vyama haimaanishi kuwa wamoja badala yake tunatengeneza migogoro, naomba tuweke nguvu kuimarisha umoja wetu ambao unatuunganisha watumishi wote na kutetea maslahi yetu," alisema Lamosai.

Kaimu Mkuu wa OTTU jijini Mbeya, Martha Lwitiko, aliwaasa viongozi wa vyama vya wafanyakazi kujenga uhusiano mzuri mahali pa kazi ili kuepusha migogoro miongoni mwa wafanyakazi na waajiri.

Berege alisema sheria ya usajili wa vyama vya wafanyakazi inaweza kubadilishwa endapo mchakato huo utaanzia kwa wafanyakazi wenyewe.

Alisema wingi wa vyama vya wafanyakazi unadaiwa hausaidii kutetea maslahi ya mfanyakazi na badala yake unazidi kuwadidimiza, hali ambayo imesababisha baadhi ya viongozi wa vyama hivyo kuiomba serikali ifanye marekibisho ya sheria kwa lengo la kupunguza idadi ya vyama vya wafanyakazi nchini.

**"Wingi wa vyama haimaanishi kuwa wamoja badala yake tunatengeneza migogoro, naomba tuweke nguvu kuimarisha umoja wetu ambao unatuunganisha watumishi wote na kutetea maslahi yetu," alisema Lamosai.**

# Mil. 400/- kujenga Kituo cha Afya Wilayani Kyela

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya kupitia mapato yake ya ndani imetenga shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ngonga.

Kituo hicho pia kitatoa huduma ya mama na mtoto, lengo likiwa ni kuwasaidia wajawazito na watoto kupata huduma kwa karibu kuliko ilivyo sasa ambapo hutumia muda na gharama kubwa kufuta huduma bora za matibabu katika Hospitali ya Wilaya hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, alisema kuwa walikubaliana ujenzi wa kituo hicho baada ya kuona madhila wanayopata wananchi wa kata za Ngoja, Katumba Songwe na Ikolo kupata huduma bora za afya.

Alisema kituo hicho kitahudumia zaidi ya wakazi 10,000 watanufaika na huduma bora za matibabu baada ya kukamilika.

"Halmashauri ya Wilaya kupitia mapato ya ndani tumetoa shilingi milioni 400 pamoja na eneo kubwa ambalo litajegwa kituo kikubwa cha afya kitakachohudumia wakazi wa Ngonga na maeneo jirani katika bajeti yetu ya mwaka 2021/2022... naamini ndani ya mwaka huu tutafikia hatua nzuri na ikiwezekana kumaliza kabisa kadri fedha zitakapopatikana pia tunawakaribisha wadau kusaidia," alisema Kingamkono.

Aliongeza kuwa katika kuboresha huduma za afya Serikali Kuu imetoa jumla ya shilingi milioni 550 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Itunge na Zahanati ya Kilasilo.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Ismail Mlawa, aliwataka madiwani kusimamia vyema miradi ya maendeleo ili wananchi wapate huduma bora na za uhakika.

Alisema Wilaya ya Kyela ni kongwe, lakini haisongi mbele kwa sababu ya kukosa uzalendo, hivyo aliwashauri viongozi hao kuungana ili kuibadilisha wilaya hiyo. Diwani wa Katumba Songwe, Fyuda Msusi, alisema miongoni mwa vipaumbele vya wilaya hiyo ni kuboresha sekta ya elimu, afya na kilimo na kwamba madiwani wamekuwa mstari kusimamia miradi inayotekelezwa.



# Zena aipa 5 taasisi kwa uhamasishaji saratani ya matiti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Zena Ahmed Said, amezitaka taasisi za afya kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Taasisi ya Wajamama Fitness Center kuhamasisha wanawake kujihadhari na ugonjwa wa saratani ya matiti.

Hayo aliyaeleza katika hafla ya uzinduzi wa matembezi ya kuhamasisha uelewa kuhusu maradhi ya saratani ya matiti yaliyofanyika jana huko Mbweni Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema saratani ni moja ya magonjwa makubwa yanayowaathiri wanawake duniani, lakini inatibika iwapo itawahiwa.

Alieleza kuwa kwa mujibu wa wataalamu wa afya, saratani ya matiti inatibika ikitambuliwa mapema, hivyo aliipongeza taasisi hiyo kwa juhudi zao na kutambua umuhimu huo wa kuwahamasisha wanawake kuchukua tahadhari ya kutambua mapema saratani hiyo.

Alieleza kuwa mwaka 2020 wanawake milioni 2.3 duniani waliathirika na saratani hiyo huku 685,000 wakipoteza maisha.

Hivyo alisema kwamba ni muhimu kuchukua tahadhari zote zinazowezekana kupunguza makali ya maradhi hiyo.

Alisema kuwa ni matarajio yake kwamba hatua hiyo itaendelea na kupewa uzito unaostahiki kwa lengo la kuokoa maisha ya wanawake ambao wangeweza kuathirika na maradhi hayo.

Naye Mkurugenzi Mkuu na Mwanzilishi wa Taasisi hiyo ya Wajamama, Nafisa Jidawi, alisema hayo ni matembezi ya pili kufanyika, ambapo mwaka jana walifanya mbio hizo na wanawake 50 waliwaelimisha na kuwapima saratani ya matiti na kwa mwaka huu wanatarajia kuwafikia wanawake 100.

# Hemed awashauri matibabu wanaopata matatizo ya akili

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

JAMII imeshauriwa kujenga utamaduni wa kuvitumia vituo vya afya, hospitali za wilaya na Hospitali ya Rufani ya Kidongo Chekundu wanapopatwa na matatizo ya akili ili kupata matibabu stahiki.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema hayo wakati akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani katika viwanja vya Mnara wa Kumbukumbu Michenzani Mjini Zanzibar.

Alisema jamii inapaswa kutumia haki yao ya msingi ya kupata matibabu kwa kufika katika vituo vya afya na kuachana na dhana ya imani potofu ya ushirikina.

'Naomba mtumie haki yenu ya kuwa na afya njema, haki ambayo inapatikana katika taasisi za serikali nilizoziainisha na zinapatikana bila ya malipo," alieleza Hemed.

Hemed alisema kwa mujibu wa ripoti mbalimbali za Shirika la Afya Duniani (WHO) kupitia machapisho yake, bado kuna changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kutibu afya ya akili ambapo serikali mbalimbali duniani huelekeza wastani ya asilimia tatu kwa ajili ya huduma za afya ya akili.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza uwekezaji katika huduma ya afya ya akili tangu mwaka 2000 ambapo Serikali ya awamu ya saba kwa mashirikiano na Norway wamejenga Hospitali maalum ya Kidongo Chekundu kwa ajili ya matibabu ya fya ya akili.

Pia alisema serikali katika kutoa msukumo, imeshapeleka wataalamu saba kusomea fani mbalimbali za matibabu ya afya ya akili ndani na nje ya nchi wakiwamo madaktari bingwa wanne na wanasaikolojia watatu.

Hemed alieleza kuwa serikali ina mpango wa kuwezesha kulazwa hospitili ya watoto wenye matatizo ya afya ya akili wenye umri kati ya miaka saba hadi minane baada ya jengo jipya litakapokamilika na kufunguliwa.

Alieleza kuwa takwimu zinaonyesha magonjwa ya akili yanachukua nafasi ya 13 miongoni mwa magonjwa makuu yanayotikisa ulimwengu ambapo kila penye watu wanne mtu mmoja ameugua tatizo la afya ya akili.

Akisoma risala kwa niaba ya wahudumu wa afya ya akili mratibu Suleiman Abdu Ali, alisema kuwa bado huduma za afya ya akili zinaathiriwa kutokana na utofauti wa mitazamo ndani ya jamii, hali ambayo inasababisha kuendelea kwa tatizo la unyanyapaa wa wagonjwa wa akili.

Aidha, Suleiman alisema wafanyakazi wa huduma za afya ya akili wanaipongeza serikali kwa kuendelea kutoa kipaumbele katika kuimarisha huduma za afya ya akili kupitia vituo mbalimbali vilivyomo katika wilaya pamoja na Hospitali ya Kidongo Chekundu.

Akizungumzia changamoto wanazokabiliana nazo, alisema udogo wa bajeti usiokidhi kufikia malengo, changamoto ya usafiri na mgongano wa sheria.

Mwakilishi kutoka Houkland University, Dk. Christina alisema ushirikiano wa pamoja kati ya SMZ na Norway katika huduma za afya ya akili ulioanza mwaka 2011, umezaa matunda kutokana na kujengwa jengo zuri la kutoa huduma za afya ya akili Zanzibar liliopo katika eneo la Kidongo Chekundu.



Baadhi ya watalii wakiteremka katika ndege ya Edelweiss kutoka Switzerland, kwa mara ya kwanza ndege hiyo, juzi imeanza safari yake ya kufika katika Viwanja vya Abeid Amani Karume Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Safari ya kwanza ya ndege yaleta Zanzibar watalii 150

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZAIDI wa watalii 150 waliwasili Zanzibar juzi kwa ndege ya Edelweiss kutoka Uswisi ambapo ndege hiyo kwa mara ya kwanza imeanza safari yake ya kuja Zanzibar.

Ndege hiyo iliyotua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar na kupokelewa kwa shangwe na nderemo ambapo ujio wa ndege hiyo ni juhudi za serikali katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar.

Akizungumza katika mapokezi hayo kwa niaba ya Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mkurugenzi Mipango na Maendeleo ya Utalii Zanzibar kutoka Kamisheni ya Utalii, Aviwa Issa Makame, alisema ujio wa ndege hiyo itaongeza pato la nchi sambamba na vijana kupata ajira mbalimbali kupitia sekta ya utalii na kuimarisha uchumi wa nchi.

Alisema mategemeo ya serikali kwa sasa ni kuendelea kupokea wageni wengi kutoka Uswisi kwa kuwa awali idadi ya wageni kutoka nchi hiyo ilikuwa ndogo kutokana na takwimu ya uingiaji wa wageni Zanzibar. Aidha, alisema kuwa kwa mujibu wa ratiba zilizopo wageni wengi kutoka Uswisi watakuwa wanaingia nchini, ambapo ndege hiyo itakuwa ikifanya safari zake mara mbili kwa wiki.

Akizungumzia soko la utalii, mkurugenzi huyo alisema kuwa kutokana na ugonjwa wa corona soko hilo, lakini kwa sasa limeanza kuimarika kutokana na juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na kukabiliana na ugonjwa huo ikiwamo utoaji wa chanjo ya corona. "Sasa soko la utalii linakuwa vizuri na watalii wengi wamekuwa wakiingia kutoka nchi mbalimbali," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mauzo wa Kundi la kampuni za Lufthansa Kusini na Mashariki mwa Afrika, Dk. Andre Schulz, alisema kundi la kampuni yake limepanua wigo wake Tanzania, ambapo litatoa huduma za ndege mara mbili kwa wiki kuunganisha kati ya miji ya Kilimanjaro, Dar es Salaam na Zanzibar kwa kutumia ndege hiyo.

Balozi wa Uswisi nchini, Pascal Moser, alisema nchi yake, itaendelea kuleta wageni kwa sababu mandhari ya Zanzibar yanamvuto wa kipekee.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Hamdani Omari Makame, alisema lengo la mamlaka ni kutanua wigo wa kuimarisha huduma kwa wananchi hasa watalii.

## HABARI KITAIFA

# Tani 1,865 korosho zakwama kuuzwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

JUMLA ya tani 1,865 za korosho zilizotarajiwa kuuzwa kupitia mnada wa kwanza wa Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao zimekwama kununuliwa kutokana na wakulima kukataa kuuza kwa bei ndogo.

Bei hiyo ambayo waliikatia ndiyo iliyokuwa imefikiwa na kampuni za ununuzi wa zao hilo zilizojitokeza.

Korosho hizo zipo katika maghala matatu ya Nangurukuru, Wilaya ya Kilwa zipo tani 702 na kilo 492 Msajili Hazina, Halmashauri ya Mtama tani 690 na kilo 606 na la Buco lililopo Manispaa ya Lindi lina tani 502 na kilo 499.

Kampuni 12 zilijitokeza kununua korosho hizo, lakini bei iliyofikiwa ya juu ilikuwa Sh. 2,270 na ya chini ilikuwa Sh. 2,010, hivyo kuwafanya wakulima kutoridhia kuuza kwa bei hiyo kwa madai ni ndogo kulingana na gharama kubwa katika uzalishaji.

Wakiwasilisha malalamiko kwa viongozi wa Bodi ya Korosho nchini, wilaya na wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutoka Mkoa wa Dar es Salaam waliohudhuria mnada huo, wakulima hao walisema kutokana na gharama kubwa za uzalishaji, hawapo tayari kuuza kwa bei hiyo.

Maimuna Yusufu, Halidi Selemani, Juma Dadi na Rehema Hemedi wakizungumza kwa niaba ya wakulima wenzao, walisema kilimo cha korosho kina changamoto nyingi zikiwamo gharama za uzalishaji wake kuanzia palizi, pembejeo, upuliziaji, uokotaji na ubebaji hadi vyama vya msingi (Amcos).

Walisema kutokana na ugumu wa kazi ya kilimo cha korosho na kushuka kwa bei inayofikiwa na wanunuzi, kunawafanya wakate tamaa kuendelea kulima korosho. Walisema lita ya dawa za kupulizia wananunua kwa Sh. 50,000 pamoja na gharama nyingine.

Aidha, walisema kuuza korosho kwa Sh. 2270 kwa kila kilo moja ni kuendelea kupoteza nguvu zao bure, ikizingatiwa wanakabiliwa na makato mbalimbali yakiwamo ya Amcos, utunzaji maghala, mfuko wa elimu, TARI na mengineyo.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi akimwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Zainabu Telak, aliwaambia wakulima hao kuwa wanaheshimu maamuzi yao, na kueleza kuwa mnada huo utafanyika siku nyingine na iwapo hali haitabadilika, watajua njia ipi ifanyike ili kuwaokoa.

## Benki yasaidia Shule Kisutu madawati 100

**Na Zuwena Shame**

SHULE ya Msingi Kisutu ya jijini Dar es Salaam, imepokea madawati 100 na vifaa mbalimbali vya kufundishia vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 10 kutoka Benki ya Canara Tanzania ikiwa ni moja kati ya sehemu ya kurudisha fadhila katika jamii na kusaidia juhudi mbalimbali za serikali kwenye sekta ya elimu.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutoa msaada huo, Mkurugenzi Mkuu benki hiyo, Balaji Rao alisema kuwa benki hiyo inatambua umuhimu na thamani ya elimu katika kujenga kizazi bora kijacho katika Taifa la Tanzania kwa sababu elimu inayotolewa ndiyo huakisi maisha ya wanafunzi ya baadaye.

Rao alisema walimu wanapaswa kutekeleza majukumu yao katika kufundisha, ufanisi wa elimu yao na ufundishaji wao una uhusiano na uwezo wa ufaulu wa wanafunzi wanaowafundisha.

"Tunaelewa kuwa uwezo wa shule kufaulu unachangiwa na sababu mbalimbali, lakini zaidi ni walimu, wanafunzi wenyewe, vifaa vya kufundishia na mazingira pia. Hivyo tumeamua kuchukua mpango huu kusaidia serikali vifaa vya kufundishia ili kuwe na uwezo wa kufaulu mkubwa katika masomo ya wanafunzi hapa shuleni," alisema Rao.

"Shuleni ndiyo sehemu tunapata watu wenye taaluma mbalimbali kama wanasheria, madaktari, wabunge na hata rais wa nchi. Hivyo kuwa na vifaa vya kufundishia vya kutosha kama madawati tutaweza kupata watu wenye taaluma wengi nchini. Tunaamini madawati haya yataweza kusaidia ufaulu na kuwa na maisha bora baadaye kwa kusoma vizuri bila vikwazo," aliongeza Rao.

Pia, aliwahamasisha wanafunzi hao kusoma kwa bidii kwa kuwa elimu ni ufunguo wa maisha.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya I&M, Baseer Mohammed (wapili kulia) na Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa benki hiyo, Donald Mate (wapili kushoto) na Mkuu wa Idara ya Wateja wa Rejareja wa benki hiyo, Lilia Mtali (kushoto), wakimkabidhi tuzo Meneja Msaidizi wa Kitengo cha Huduma za Kidigitali, Sabas Bunchikuli, katika hafla ya siku ya wateja wa benki hiyo, jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara Mwenge walalamikia kuwekewa uzio

**Na Beatrice Shayo**

WAFANYABIASHARA wa eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuwasaidia kuondolewa kwa uzio uliowekwa kwa sasa kwa kuwa unazuia wateja kufika katika maduka yao hali inayosababisha kushindwa kufanya biashara.

Wafanyabiashara hao jana wakizungumza na waandishi wa habari wamelalamikia uzio huo ambao umewekwa hivi karibu baada ya kuondolewa mabati, unazuia wateja na usalama mdogo iwapo itatokea ajali.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara hao, Maganga Wilson, alisema wamesikitishwa na uamuzi wa kuwazungushia ukuta wa chuma ambao wateja wao wanashindwa kuingia madukani.

"Tumekaa miaka mitatu tunafanya biashara katika mazingira magumu walivyotuwekea uzio wa mabati kwa sababu ya umuhimu wa ujenzi uliokuwa unaendelea wa barabara ilitubidi tuvumilia ila kwa sasa wametoa mabati wametuwekea chuma. Tunamwomba Rais Samia atusaidie kuna mchezo unaoendelea hapa," alisema.

"Hili ni eneo la biashara manispaa wanatakiwa kuliangalia hatuwezi kulipa leseni halafu wanasababisha kutufungia biashara hili haliwezi kukubalika tumeumia kwa miaka mitatu wametoa uzio wa bati tukafurahi kuwa tutaanza kupata wateja matokeo yake wameweka wa chuma wangeacha njia ya wateja kupita kuja ndani katika maduka yetu."

Alisema kama manispaa inataka eneo hilo wangeweka kote uzio wa chuma walipotoa mabati badala ya kufungia wateja wasipite katika maduka yao.

"Sisi tunahangaika kutafuta riziki ya siku na watu hawataki tutaishi vipi tunaomba Rais atusaidie sisi wafanyabiashara eneo la Mwenge linakuwa ni kero," alisisitiza.

Naye Joyce Kessy alisema wateja kufika katika duka lake imekuwa ni changamoto kutokana na uzio uliowekwa hivi karibuni.

Alisema uzio huo ungetoa njia kwa ajili ya wateja kuingia katika maduka yao na sio walivyofanya kufunga njia na kuwasababishia kushindwa kufanya biashara.

Alisema serikali inawataka walie kodi ingawa inawaweka mazingira magumu katika ufanyaji wa biashara jambo ambalo linawaumiza kushindwa kuendelea kiuchumi.

"Ikitokea tumepata ajali ya moto madhara yatatokea makubwa kwa kuwa uzio huo hakuna njia ya kutoka hii ni hatari waangalie namna ya kutusaidia tuna maduka kama 108 wamezuia biashara zetu kutokana na uzio huu mpya wa chuma," alisema.

Akifafanua suala hilo, Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge, alisema atalifanyia kazi ili wafanyabiashara hao wasifanye shughuli zao kwenye mazingira magumu.

HABARI MICHEZO

# SBL YAIPONGEZA STARS KWA USHINDI

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), kupitia bia yake ya Serengeti Lager, ambayo ni mdhamini mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, imekipongeza kikosi cha timu hiyo kwa kuibuka na ushindi ugenini dhidi ya Benin, ulioiwezesha kurudi kileleni mwa msimamo wa Kundi J katika michuano ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia Qatar 2022.

Katika mechi hiyo ya marudiano iliyopigwa Uwanja wa L'Amitie, Cotonou nchini Benin juzi, Jumapili, Simon Msuva aliutendea haki mpira wa kurushwa kutoka kwa Israel Mwenda, baada ya kuwapiga chenga walinzi kadhaa wa wapinzani wao na kisha kuachia shuti kali lililojaa moja kwa moja wavuni na kuifanya Stars kuibuka na ushindi wa bao 1-0, hivyo kukaa kileleni ikiwa na pointi saba sawa na Wabenin hao, lakini Tanzania ikifaidika na idadi kubwa ya mabao ya kufunga.

Licha ya Benin kuichachafia Stars ikitaka kusawazisha bao hilo la mapema dakika ya saba, mabeki walikuwa imara kulinda lango lao huku timu ikibadili mfumo na kutumia mashambulizi ya kushtukiza ambayo yalikuwa hatari kwa wenyeji hao.

Akizungumza na mwandishi wetu jana kuhusu ushindi huo, Meneja Chapa wa Bia wa SBL, Wankyo Marando, alisema wamefurahishwa na ushindi huo wa Taifa Stars na kuongeza kuwa kama ambavyo wamekuwa wakifanya wataendelea kuiunga mkono timu hiyo na kusisitiza kuwa Tanzania ina nafasi ya kufanya vizuri na kushiriki fainali hizo kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwake mwaka 1930.

"Tunaipongeza Taifa Stars kwa kiwango kizuri ilichoonyesha kwenye mechi dhidi ya Benin, tukiwa kama wadhamini wakuu wa timu hii, tumefurahishwa na kiwango ilichoonyesha na kuweza kuifunga timu ngumu kama Benin kwenye uwanja wao wa nyumbani. Tunaamini Taifa Stars itaendelea kufanya vizuri katika mechi zake dhidi ya Madagascar na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo," alisema Wankyo

Aliongeza "SBL inaendelea kuiunga mkono timu yetu ya taifa kwa sababu tunaamini inaweza kufanya vizuri. Tunafahamu kuwa kufuzu kucheza Kombe la Dunia siyo jambo rahisi, lakini jitihada za wachezaji pamoja na timu nzima zina kila sababu ya kutufanya tuamini kuwa inawezekana.

"Tukumbuke kuwa Taifa Stars iliweza kufuzu kushiriki michuano ya mashindano ya Mataifa ya Afrika nchini Misri mwaka 2019 ikiwa ni baada ya miaka 38, hii inaonyesha kuwa inaweza kutupeleka kwenye Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza".

Meneja huyo wa chapa, alisema Bia ya Serengeti itaendelea kuiunga mkono Taifa Stars na kuwa shabiki namba moja wa timu hiyo huku akiwataka mashabiki na Watanzania kwa ujumla kuendelea kujivunia vya nyumbani ikiwa ni pamoja na timu yao na bia yao ya Serengeti.

"Chapa ya Serengeti ni mdau mkubwa wa michezo hapa nchini na tunaona furaha kuchangia maendeleo ya michezo na tunaahidi kuendelea kuhamasisha na kuchangia maendeleo ya sekta hii ambayo pia huwaleta watu pamoja," alisema.

Mwaka jana, Bia ya Serengeti Premium Lager iliingia mkataba wa miaka mitatu na TFF na kuwa mdhamini mkuu wa Taifa Stars kwa makubaliano ya kutoa kiasi cha shilingi bilioni tatu katika kipindi cha mkataba. Mkataba huo ulikuja baada ya kumalizika kwa mkataba wa awali ambao pia ulikuwa ni wa miaka mitatu uliosainiwa mwaka 2017.

SBL kupitia bia yake pendwa ya Serengeti Lite pia ni mdhamini mkuu wa Ligi ya Wanawake ikiwa ni mdhamini wa kwanza na wa pekee wa ligi hiyo tangu kuanzishwa hapa nchini.




Mshambuliaji wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, akimchekecha mlinzi wa Benin. Stars juzi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 ugenini dhidi ya Benin kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia Qatar 2022. **PICHA: MAKTABA**

# Poulsen: Tanzania inaweza kwenda Qatar

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Kim Poulsen, amesema ndoto ya kila Mtanzania ni kuona kikosi hicho kikicheza fainali za Kombe la Dunia, hasa baada ya ushindi wa juzi wa bao 1-0 dhidi ya Benin ugenini, akiongeza kuwa nafasi ipo wazi kwao.

Akizungumza baada ya mechi ya Kundi J kwenye Uwanja wa L'Amitie, Cotonou nchini Benin, kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar, Poulsen alisema kucheza fainali za Kombe la Dunia ni jambo linalowezekana kwa Stars, huku akieleza kuwa nafasi iko wazi kwa nchi za Benin, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Tanzania pia.

"Kucheza fainali za Kombe la Dunia kwa Tanzania inawezekana kwa sababu matokeo haya yanalifanya kundi kuwa wazi na timu yoyote ile kati ya Benin, DR Congo na Tanzania moja wapo inaweza kuongoza kundi na kwenda kwenye hatua ya mtoano," alisema kocha huyo ambaye Alhamisi iliyopita alishuhudia timu yake ikipoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Wabenin hao.

Kiufundi alisema kuwa alibadilisha mbinu kwenye mechi hiyo, tofauti na ile ya kwanza.

"Tulibadilisha mbinu, tulijifunza kwenye mechi ya kwanza, niliweka mastraika matatu, niliweka pia mabeki watatu, Kennedy Juma, Dickson Job na Bakari Mwamnyeto na hii ni kwa ajili ya kucheza mipira ya juu, kwani waliitumia sana na yule mchezaji wao namba tisa alikuwa mzuri kwa mipira hiyo, hivyo nilimwekea watu wa kumdhibiti," alisema.

Alisema haikuwa mechi rahisi kwa sababu Benin ilikuwa kwao, mbele ya mashabiki wake, lakini pia ina ubora mkubwa kwenye viwango vya soka ulikilinganisha na Tanzania, hivyo aliwapongeza vijana wake kwa kupambana kwa ajili ya taifa.

Wakati huo huo, Tanzania imeendelea kuwa kinara kwenye kundi hilo baada ya timu iliyoonekana tishio kwenye nafasi hiyo, DR Congo kuchapwa bao 1-0 ugenini dhidi ya Madagascar.

Kwa matokeo hayo, Stars inaongoza kwa kuwa na pointi saba kama Benin, lakini ina mabao matano ya kufunga, ikifungwa manne, huku Benin ikifunga matatu na kufungwa mawili.

## Tambwe fiti kuivaa African Sports

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa DTB FC, Amissi Tambwe, ameanza mazoezi na yuko fiti kwa mchezo ujao wa Ligi Daraja la Kwanza dhidi ya African Sports unaotarajiwa kuchezwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Tambwe aliumia na kushindwa kuendelea kwenye mchezo dhidi Green Warriors uliopigwa Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa Mej Gen. Isamuyo, Mbweni jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Muhibu Kanu, alisema baada ya kupata matibabu nyota huyo amerejea mazoezini na yuko fiti kwa ajili ya mchezo unaofuata dhidi ya African Sports.

## Kunenge azindua 'Jogging' Chalinze

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge, amewashauri wananchi kuiga mfano wa Rais mstaafu, Jakaya Kikwete, katika kufanya mazoezi ili kujikinga na magonjwa mbalimbali.

Kunenge aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizindua rasmi kikundi cha mazoezi ya kukimbia 'Jogging', wilayani Chalinze, ambapo alisisitiza wananchi kujiwekea utaratibu wa kufanya mazoezi ili kuwasaidia katika kuimarisha afya na kujikinga na magonjwa.

Naye Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, aliwashukuru wote walioungana pamoja katika uzinduzi huo wa mazoezi ili kutunza afya zao.

## ZISIKUPITE

### NEWCASTLE KUIBOMOA UTD

KLABU ya Newcastle United itawalenga wachezaji wanne wa Manchester United wakati dirisha la uhamisho litakapofunguliwa Januari huku mshambuliaji wa Ufaransa, Anthony Martial, 25, kiungo wa kati wa Uholanzi Donny van de Beek, 24, beki wa Ivory Coast Eric Bailly na mshambuliaji wa England, Jesse Lingard, 28, wote wakiwa katika orodha yao. ***(Mirror)***

### HAALAND ATAKIWA BARCA

MAKAMU wa Rais wa Klabu ya Barcelona, Rafael Yuste, amepuuza fursa ya klabu hiyo ya Hispania kumsajili mshambuliaji hatari wa Borussia Dortmund raia wa Norway, Erling Braut Haaland, 21. ***(Mundo Deportivo)***

### NEYMAR AANZA KUAGA

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Neymar, 29, amesema huenda Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar ikawa michuano yake ya mwisho, kwa sababu mshambuliaji huyo wa PSG hana uhakika iwapo akili yake ina uwezo wa kukabiliana na changamoto za soka. ***(DAZN, via Goal)***

### BARCA KUMUUZA DEMBELE

KLABU ya Barcelona huenda ikamuuza winga wa Ufaransa, Ousmane Dembele, 24, iwapo mchezaji huyo hatoongeza mkataba wake na pengine klabu hiyo ya Hispania ikajaribu kumsajili mshambuliaji wa Manchester City na England, Raheem Sterling, 26. ***(Sport)***

### RAMSEY KUGEUZWA CHAMBO

JUVENTUS itamtumia kiungo wa kati wa Wales, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 30 kama chambo cha kumvutia kiungo wa kati wa Manchester United na nyota wa Ufaransa, Paul Pogba, 28, kurudi mjini Turin. ***(Mail)***

### ATAKIWA NEWCASTLE

WAMILIKI wapya wa klabu ya Newcastle United wana mpango wa kumbadilisha kocha wa klabu hiyo na kumchukua yule wa Leicester City, Brendan Rodgers. ***(Mail)***

### MCKENNIE AWINDWA SPURS

KLABU ya Tottenham inahusishwa na jaribio la kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Marekani, Weston McKennie, 23, na mchezaji wa Uswis, Dejan Kulusevski, 21, kutoka Juventus. ***(Calciomercato, via Teamtalk)***


### MORATA AWANIWA SPURS

TOTTENHAM inamnyatia mshambuliaji wa Hispania, Alvaro Morata, 28, kuchukua nafasi ya Harry Kane, 28. Morata kwa sasa yuko Juventus kwa mkopo akitokea Atletico Madrid. ***(Fichajes)***

### CHRISTENSEN KUULA CHELSEA

KLABU ya Chelsea imekubali kumpa mkataba mpya kiungo wa kati wa Denmark, Andreas Christensen, huku makubaliano hayo yakiendelea kukamilishwa kabla ya kutangazwa rasmi. ***(Fabrizio Romano on Twitter)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI ATOA YA MOYONI KUONDOKA BARCELONA

●●● Nilikuwa nimerudi Hispania baada ya michuano ya Copa America Julai, nilichokuwa nakiwaza ni...

**BUENOS AIRES,** Argentina

LIONEL Messi ametoa ya moyoni jinsi alivyolazimika kuondoka Barcelona katika mazingira ya kulazimishwa na ambayo hakuyatarajia kwenye mahojiano na CNN.

Messia aliondoka Barcelona na kujiunga na PSG ya Ufaransa kwa uhamisho huru baada ya Barcelona kushindwa kumwongezea mkataba kutokana na matatizo ya kifedha.

Katika mahojiano na Kituo cha Televisheni cha CNN, Messi ameamua kupasua jipu kwa kusema ukweli kile kilichotokea.

**"Nilikuwa nimerudi Hispania baada ya michuano ya Copa America Julai, nilichokuwa nakiwaza ni kwamba mkataba huo uliwekwa pembeni kwa sababu saini yangu tu ndio ilikuwa inasubiriwa kumbe sivyo.**


"Nilipowasili Barcelona niliambiwa hilo la kusaini mkataba mpya haliwezekani tena, hivyo nitafute klabu nyingine kwa sababu hawawezi kuniongezea mkataba.

"Hilo lilinipa wakati mgumu sana nikaanza kufikiria mengi ikiwamo kubadilisha mfumo wa familia yangu kuacha makazi na kwenda kuanza upya sehemu nyingine.

"Kujiunga na PSG sikukosea, kilichonisaidia mimi kutulia baada ya kujiunga na PSG ni sura ninazozifahamu hapo na kuzingatia kwamba kuna wachezaji wengi wanaoongea lugha ya Kihispania kama 'Ney' 'Lea' (Paredes), 'Fideo' (Di Maria)," alisema Messi ambaye hadi sasa ameifungia bao moja tu PSG tangu ajiunge nayo kipindi cha majira ya joto.

MECHI KALI
HOME
ZIMBABWE
8.84 | 3.39 | 1.69
GHANA
AWAY
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa
CHEZA USHINDE
JACKPOT
TZS. 576

# POGBA HAJUI HATIMA YAKE



**MANCHESTER,** England

PAUL Pogba bado yupo kwenye hali ya 'sintofahamu' kuhusu kusaini mkataba mpya na Klabu ya Manchester United.

Pogba amekuwa katika hali ya kusubiri kwa majuma kadhaa, huku akiwataka viongozi wa klabu hiyo kumpa muda na jibu kubwa analolitoa kila mara kwa kusema "ngoja tusubiri tuone nini kitatokea baadaye."

Hali hiyo inaendelea kutoa mwanya kwa wadau wa soka duniani kuhisi huenda kiungo huyo akaikacha Manchester United mwishoni mwa msimu huu, kutokana na kuhusishwa na mpango wa kuwaniwa na klabu za Juventus na Real Madrid.

Taarifa za hivi karibuni zilibainisha kwamba, huenda Pogba akaongeza mkataba mpya na 'Mashetani Wekundu' hao, kutokana na mkataba wa sasa kutarajiwa kufikia kikomo mwishoni mwa msimu huu.

Ripoti hiyo imeeleza kwamba, kusajiliwa kwa Cristiano Ronaldo na Jadon Sancho kumemfanya Pogba ashawishike kubakia klabuni hapo, lakini bado hajafanya maamuzi ya kusaini mkataba mpya.

Hata hivyo, akizungumza baada ya ushindi dhidi ya Ubelgiji, Pogba aliiambia Sport Mediaset: "Mara zote huwa nazungumza na wachezaji wenzangu wa zamani kama Paulo (Dybala).


# Ufaransa mabingwa wapya Uefa

**PARIS,** Ufaransa

TIMU Taifa ya Ufaransa, 'Les Bleus', imefanikiwa kutwaa ubingwa wa mashindano ya Ligi ya Mataifa ya UEFA baada ya kutokea nyuma na kuwafunga Hispania mabao 2-1 juzi.

Hispania walikuwa bora katika kipindi cha kwanza, lakini hadi mapumziko timu hizo zilikuwa hazijafungana, huku kipa na nahodha wa Ufaransa, Hugo Lloris, akionyesha ukomavu mkubwa kwa kuokoa hatari nyingi.

Kipindi cha pili kilikuwa bora zaidi kwa Ufaransa ambapo walicheza vizuri, lakini Hispania walikuwa wakwanza kumsalimu Lloris kwa bao bora kabisa kutoka kwa mshambuliaji Mikel Oyarzabal dakika ya 64 ya mchezo.



Dakika mbili baadaye mshambuliaji Karim Benzema aliwarudisha mchezoni Les Bleus, kabla ya Kylian Mbappe kuwahakikishia ushindi dakika ya 80 ya mchezo.

Hivyo, rasmi sasa Ufaransa wametangazwa mabingwa wa Ligi ya Mataifa ya UEFA (Uefa Nations League) wakichukua ufalme huo kutoka kwa timu ya Taifa ya Ureno.

## HABARI MICHEZO


# 6,086,780

# JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 16/10/21 | 17:00 | Southampton vs Leeds | 2.40 | 3.52 | 2.82 |
| 02. 16/10/21 | 17:00 | Blackburn vs Coventry | 2.81 | 3.11 | 2.52 |
| 03. 16/10/21 | 17:00 | Millwall vs Luton Town | 2.30 | 3.20 | 3.06 |
| 04. 16/10/21 | 17:00 | Girona vs Huesca | 2.44 | 2.87 | 3.16 |
| 05. 16/10/21 | 19:15 | Las Palmas UD vs Tenerife | 2.51 | 2.95 | 2.95 |
| 06. 16/10/21 | 19:30 | Levante vs Getafe | 2.56 | 2.91 | 3.11 |
| 07. 16/10/21 | 21:30 | Malaga vs Zaragoza | 2.53 | 2.97 | 2.92 |
| 08. 17/10/21 | 13:30 | Cagliari vs Sampdoria | 2.72 | 3.37 | 2.56 |
| 09. 17/10/21 | 14:00 | Swansea vs Cardiff | 2.44 | 3.06 | 2.96 |
| 10. 17/10/21 | 16:00 | Everton vs West Ham | 2.38 | 3.42 | 2.92 |
| 11. 17/10/21 | 16:00 | Bordeaux vs Nantes | 2.78 | 3.13 | 2.59 |
| 12. 17/10/21 | 16:00 | Udinese vs Bologna | 2.36 | 3.35 | 3.00 |
| 13. 17/10/21 | 17:00 | Leganes vs Valladolid | 2.46 | 2.97 | 3.02 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 12 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:14 | 1800 | Japan vs Australia | 1.94 | 3.14 | 3.82 |
| 16:00 | 4030 | Namibia vs Senegal | 15.42 | 5.78 | 1.17 |
| 16:00 | 4630 | Zimbabwe vs Ghana | 4.84 | 3.39 | 1.69 |
| 16:30 | 4742 | Iran vs South Korea | 2.11 | 2.89 | 3.62 |
| 17:00 | 3881 | Kazakhstan vs Finland | 4.62 | 3.27 | 1.86 |
| 17:30 | 4648 | Poland U21 vs San Marino U21 | 1.01 | 19.40 | 43.66 |
| 18:00 | 1120 | Iceland U21 vs Portugal U21 | 12.61 | 6.40 | 1.16 |
| 18:00 | 4727 | Ukraine U21 vs Faroe Islands U21 | 1.07 | 8.90 | 19.35 |
| 18:00 | 5291 | Bulgaria U21 vs Switzerland U21 | 3.53 | 3.48 | 1.91 |
| 18:30 | 1805 | Hungary U21 vs Germany U21 | 7.93 | 5.22 | 1.29 |
| 18:30 | 4267 | Italy U21 vs Sweden U21 | 1.53 | 4.15 | 5.02 |
| 18:30 | 4654 | Lithuania U21 vs Russia U21 | 16.40 | 6.75 | 1.13 |
| 19:00 | 1564 | South Africa vs Ethiopia | 1.39 | 4.16 | 7.35 |
| 19:00 | 3549 | Syrian Arab Republic vs Lebanon | 1.95 | 3.15 | 3.78 |
| 19:00 | 3880 | Cyprus U21 vs Greece U21 | 3.11 | 3.35 | 2.11 |
| 19:00 | 4062 | Congo vs Togo | 2.14 | 2.76 | 3.77 |
| 19:00 | 4282 | Oman vs Vietnam | 1.56 | 3.63 | 5.62 |
| 19:00 | 4823 | Czech Republic U21 vs Kosovo U21 | 1.16 | 6.17 | 14.47 |
| 19:00 | 4847 | Niger vs Algeria | 28.07 | 8.32 | 1.06 |
| 19:00 | 5294 | Norway U21 vs Estonia U21 | 1.01 | 13.58 | 48.51 |
| 19:30 | 1673 | Serbia U21 vs France U21 | 4.07 | 3.63 | 1.74 |
| 19:30 | 4188 | Azerbaijan U21 vs Croatia U21 | 13.57 | 6.79 | 1.14 |
| 19:45 | 2780 | United Arab Emirates vs Iraq | 2.03 | 3.20 | 3.45 |
| 20:00 | 3590 | Saudi Arabia vs China | 1.39 | 4.16 | 7.35 |
| 21:00 | 1771 | Belgium U21 vs Denmark U21 | 1.54 | 4.06 | 5.03 |
| 21:00 | 2409 | Newport vs Arsenal U21 | 1.98 | 3.54 | 3.25 |
| 21:00 | 2624 | Forest Green vs Brighton U21 | 1.67 | 3.97 | 4.07 |
| 21:00 | 5533 | Netherlands U21 vs Wales U21 | 1.18 | 6.19 | 11.61 |
| 21:45 | 1090 | Faroe Islands vs Scotland | 10.01 | 5.21 | 1.30 |
| 21:45 | 1110 | Yeovil vs Altrincham | 2.19 | 3.50 | 3.10 |
| 21:45 | 1124 | Sweden vs Greece | 1.84 | 3.51 | 4.31 |
| 21:45 | 1273 | Kosovo vs Georgia | 2.19 | 3.10 | 3.55 |
| 21:45 | 1431 | Grantham Town vs Matlock Town | 4.00 | 3.90 | 1.80 |
| 21:45 | 1473 | Portsmouth vs Sutton United | 1.96 | 3.54 | 3.30 |
| 21:45 | 1603 | Denmark vs Austria | 1.51 | 4.21 | 6.21 |
| 21:45 | 1824 | Israel vs Moldova | 1.16 | 7.02 | 17.06 |
| 21:45 | 2152 | San Marino vs Andorra | 5.61 | 3.36 | 1.71 |
| 21:45 | 2729 | England vs Hungary | 1.19 | 6.24 | 17.33 |
| 21:45 | 3014 | Albania vs Poland | 3.61 | 3.21 | 2.12 |
| 21:45 | 3044 | Witton Albion vs Ashton Utd | 2.16 | 3.40 | 2.96 |
| 21:45 | 3686 | Serbia vs Azerbaijan | 1.16 | 7.37 | 16.94 |
| 21:45 | 4009 | Bulgaria vs Northern Ireland | 2.77 | 2.97 | 2.77 |
| 21:45 | 4149 | Portugal vs Luxembourg | 1.08 | 10.07 | 30.22 |
| 21:45 | 4196 | Merstham vs Margate | 2.48 | 3.46 | 2.48 |
| 21:45 | 4224 | Ukraine vs Bosnia and Herzegovina | 1.77 | 3.65 | 4.51 |
| 21:45 | 4256 | Peterborough Sports vs Lowestoft Town | 1.22 | 6.22 | 8.55 |
| 21:45 | 4667 | Spain U21 vs Northern Ireland U21 | 1.05 | 9.71 | 26.21 |
| 21:45 | 4858 | Lithuania vs Switzerland | 13.08 | 6.44 | 1.21 |
| 22:00 | 3551 | Guinea vs Morocco | 5.82 | 3.49 | 1.57 |
| 23:10 | 1281 | CA Tigre vs Mitre SdE | 1.51 | 3.67 | 6.17 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# NEYMAR AJITABIRIA MWISHO WAKE




**SAO PAULO,** Brazil

NEYMAR anatarajia michuano ijayo ya Kombe la Dunia nchini Qatar itakuwa ya mwisho kwake kucheza soka kwa sababu hadhani kama ataweza kuendelea na mchezo huo.

Brazil maafuru kama Selecao wapo kwenye nafasi nzuri ya kufuzu kuelekea Qatar kutokana na kuongoza kundi lake baada ya kushinda mechi zote tisa ilizocheza hadi sasa.

Kwa Neymar, michuano ya Qatar itakuwa ni ya tatu kwake kwenye Kombe la Dunia, akiwa amecheza ile ya mwaka 2014 na 2018.

Ingawa mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain ameshinda Kombe la Shirikisho mwaka 2013 na medali ya Olimpiki mwaka 2016, atafikisha miaka 34 wakati michuano ya Kombe la Dunia itakayoandaliwa na Canada, Mexico na Marekani mwaka 2026.

Na nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, amesema anaamini michuano ya mwakani itakuwa ya mwisho kwake.

"Naiona michuano ya Kombe la Dunia 2022 ni kama ya mwisho kwangu kwa sababu sidhani kama nitaweza kuendelea kucheza soka tena. "Hivyo, nitafanya kila kitu kuhakikisha nchi yangu inafanya vizuri, na natumaini nitafanya vizuri."

Neymar amefunga mabao 69 katika mechi 113 kwa Brazil tangu alipoanza kuichezea nchi hiyo kwa mara ya kwanza dhidi ya Marekani Agosti mwaka 2010.




# *Van Gaal awatetea Koeman, De Jong*

**AMSTERDAM,** Uholanzi

LOUIS van Gaal amemtetea Kocha wa Barcelona, Ronald Koeman na kiungo Frenkie de Jong akidai kuwa wageni mara zote huwa wanalaumiwa klabu ikiwa na matatizo.

Ilionekana kwamba Koeman angefukuzwa kazi baada ya Barca kufungwa mabao 2-0 na Atletico Madrid Oktoba 2, mwaka huu na kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kulala 3-0 dhidi ya Benfica na Bayern Munich.

Hata hivyo, Rais wa Barcelona, Joan Laporta, ameamua kumbakiza kocha huyo wa zamani wa Everton.

Na kiungo De Jong alitetea hali ya klabu hiyo hivi karibuni akisema kwamba, msimu bado ni mrefu na kwamba timu hiyo hiyo inaweza kufanya vizuri.

Kocha wa Uholanzi, Van Gaal ambaye alitwaa mataji mawili ya LaLiga, Kombe la Mfalme (Copa del Rey) na UEFA Super katika muda wake wa kwanza kuinoa Barca, alikabiliwa na wakati mgumu wa mahusiano na mashabiki na wachezaji hapo Camp Nou.

Na sasa amesema kuwa hashangazwi kuona Koeman naye atakabiliwa na wakati mgumu pale Barca.

"Kila kitu kinakwenda sawa, na kuna mchango mkubwa kutoka kwa Frenkie kwani amekuwa na kiwango bora kabisa," alisema akinukuliwa na Sky Sport.

# Michezo

Jumanne Oktoba 12, 2021

Nipashe





Messi atoa ya moyoni kuondoka Barca UKURASA 21




Ibrahim Ajibu

# GOMES AHOFIA MUGALU, SAKHO KUIKOSA GALAXY

## ●●● Ni katika mechi ya CAF J'pili, Kanoute, Kapombe fiti, Ajibu, Varane gari limewaka...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Jumapili wiki hii, Simba ikitarajia kuanza kurusha karata yake ya kwanza kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, itakaposhuka dimbani ugenini nchini Botswana kuivaa Jwaneng Galaxy, hofu ya kuwakosa nyota wake wawili muhimu imetanda.

**Simba ambayo ni miongoni mwa timu zitakazoanzia raundi ya kwanza kwenye michuano hiyo msimu huu, itaanzia ugenini kabla ya timu hizo kurudiana baada ya wiki moja.**

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema hana uhakika wa kuwatumia mshambuliaji Chris Mugalu na kiungo Pape Ousmane Sakho katika mchezo huo, kutokana na kuendelea kuwa nje ya uwanja wakiuguza majeraha.

Lakini Gomes alisema Sadio Kanoute na Shomary Kapombe, ambao nao walikuwa majeruhi, tayari wamerejea mazoezini, lakini Mugalu na Sakho wanaendelea kuwa chini ya uangalizi wa daktari na ataendelea kuwafuatilia kuona kama watakuwa tayari kuivaa Jwaneng Galaxy Jumapili.



Gomes alisema Kanoute na Kapombe wapo fiti na jana walikuwa miongoni mwa wachezaji waliocheza mechi ya kirafiki ya mazoezi dhidi ya Cambiaso Sports wakati timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1.

"Kanoute na Kapombe tayari wamerejea mazoezini bado Mugalu na Sakho, tunaendelea kufuatilia afya zao kujua kama tutaweza kuwatumia katika mchezo ujao dhidi ya Galaxy ama la," alisema kocha huyo.

Alisema wachezaji waliokuwa katika majukumu na timu zao za taifa wataanza kuripoti mazoezini leo kuendelea na programu na wenzao kabla ya kuifuata Galaxy wiki hii.

Simba ambayo siku tatu zilizopita ilicheza mechi ya kirafiki ya kimazoezi na Cambiaso Sports na kuibuka na ushindi wa mabao 4-1, jana ilirudiana tena na timu hiyo katika Uwanja wa Boko Veterans na timu hiyo kutoka sara ya bao 1-1.

Alikuwa ni beki wa kati wa Simba, Henock Inonga 'Varane', aliyewaweka mbele kwa bao la kichwa dakika ya 19 akiunganisha mpira wa adhabu ndogo uliopigwa na Ibrahim Ajibu ambaye katika mchezo huo alionyesha kiwango cha kuvutia.

Kipindi cha pili Gomes alifanya mabadiliko kwa kuwatoa Ajibu, Gadiel Michael, Jonas Mkude, Said Norshad, Ally Salum na Mzamiru Yassin huku nafasi zao zikichukuliwa na Yussuf Mhilu, Kanoute, Kapombe, Jeremiah Kisubi na Abdul Swamad Kassim.

Kikosi cha Simba kilichoanza katika mechi hiyo ni Beno Kakolanya, Said Norshad, Gadiel Michael, Erasto Nyoni, Honock Inonga, Mkude, Hassan Dilunga, Mzamiru, Jimmyson Mwanuke, Ajibu na Bernard Morrison.

# Mayele aahidi ubingwa wa Ligi Kuu Yanga

**Na Adam Fungamwango**

MFUNGAJI pekee wa bao kwenye mechi ya kirafiki kati ya Yanga na JKU ya Zanzibar, Fiston Mayele, amesema anaamini ligi msimu huu itakuwa nzuri kwao na wana uwezo wa kuchukua ubingwa huo.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Mayele, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo aliyesajiliwa msimu huu kutokea AS Vita Club ya huko, alisema wao kama wachezaji wamejipanga kuchukua ubingwa na hakuna kitu kingine.

"Najisikia vizuri kufunga bao, ni mechi ya kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya ligi. Ni ligi ngumu, lakini nadhani itakuwa nzuri kwetu. Sisi tunataka kuchukua ubingwa, hakuna kingine," alisema.

Naye beki wa kati Abdallah Shaibu 'Ninja', alisema kupata mechi za kirafiki wakati huu wa mapumziko ya Kalenda za FIFA kwa wachezaji ambao hawapo kwenye vikosi vya timu ya taifa, inawasaidia kuwaweka vizuri kwa utimamu wa kimwili ili ligi ikirejea wasiwe kama wanaanza upya.

"Kupata mechi kama hizi inatupatia kitu, tunakuwa fiti wakati ligi imesimama. Nawaambia tu wanachama na mashabiki wa Yanga wiki ijayo mechi za ligi zinarejea wazidi kutupa sapoti popote pale tunapokwenda," alisema.

Yanga, Jumamosi ijayo, itakuwa kwenye Uwanja wa Majimaji Songea, mkoani Ruvuma kucheza na KMC, ambayo imeamua kupeleka huko mechi yao ya nyumbani ya Ligi Kuu Tanzania Bara.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >